# *UKRISTO DHIDI YA UABUDU SANAMU*

Hiki ni chako. Kitu hiki kidogo kwa ajili ya mama. Mpe hicho nanii . . . ? . . . Kisha kitengenezwe halafu ninii hiki kidogo . . . ? . . .

Asante, Ndugu Neville, Bwana akubariki.

Habari za asubuhi, marafiki. Ni upendeleo kurudi maskanini tena asubuhi ya leo, tukijisikia vizuri na wenye afya. Juzi hata nisingeweza kuzungumza. Nilikuwa na kijidudu hiki kidogo kinachoenea, mwajua, kinaingia kwenye koo zao na kuwafanya kupwelewa na sauti, bali Bwana alinisaidia na kunikomboa na hali hiyo kusudi niweze kuwazungumzia asubuhi ya leo.

2 Nasi tuna furaha kwamba kuna maskani nzuri iliyojaa kabisa na watu wanasimama. Laiti tu tungalikuwa na viti vingine, na kuwapa hao watu wanaosimama. Tungekuwa na furaha kama tungalikuwa navyo, lakini nafikiri kila kitu kimechukuliwa. Ninajua msingetaka kuja na kuketi pamoja na watoto hawa madhabahuni na kugeuza mgongo wako upande huu mwingine.

3 Sasa, imekuwa ni kwa siku chache ambazo nimekuwa nikisoma kwenye historia, nami niliwazia labda asubuhi ya leo badala ya kuhubiri ningeweza tu kufundisha kidogo juu ya Neno la Mungu. Na sasa huenda tukachelewa kidogo, kwa hiyo nitaninii . . . baadhi yenu mngebadilishana na hao waliosimama, ama chochote kile, hakika lingekuwa ni jema kama mngeweza—kama mngeweza kufanya hivyo na kuwapumzisha kidogo.

4 Na sasa wengi wa marafiki, wa marafiki zangu wanakuja, baadhi yao kutoka mbali sana, huko chini kabisa Georgia, huko Ohio, Tennessee, mahali mbalimbali tu, Illinois, Missouri, Michigan, wanashuka kutoka Chicago, wanatoka tu kuja kwenye mkutano mmoja wa maskani ndogo kama hii. Linanifanya kushukuru sana kwa ajili ya watu kama hao. Na si hilo tu, bali ningetaka kusema jambo hili, sio kwa manufaa ya . . . bali kwa manufaa ya Neno la Mungu: karibu kila mmoja wa hao watu hawaji tu bali wanakuja pamoja na zaka zao kuzileta kanisani kwa usaidizi.

5 Sasa, hao ni marafiki tu walio waaminifu. Kamwe huwezi kuwasahau watu kama hao.

6 Na halafu wakati mwingine labda inanibidi kusema jambo linalowararua vipande-vipande, bali mnaona linalomaanisha basi. Moyoni mwako hutaki kufanya hivyo, bali hata hivyo kuna

Kitu kinachosema, “Wewe . . . halina budi kutendwa,” mnaona, kwa hiyo huna budi kufanya hivyo.

7 Na kuwaona wakija kutoka kila mahali na—na kujaribu kumtumikia Bwana, na wakiamini katika huduma ambayo Bwana amenipa mimi na kuniamini kuwa ni mtumishi Wake kwamba nisingeweza kuwaambia jambo lolote la kimakosa, basi kwa uaminifu mkamilifu kweli sina budi kufanya yote nijuayo kufanya ku—kuzichunga nafsi za watu hao; nikijua ya kwamba hawaji hapa wapate tu kuonekana, wakiendesha magari kuivuka milima yenye barafu na vilima, na kushuka kupitia kwenye barabara zilizojaa misongamano ya magari, huku watoto wao wakikosa chakula na usingizi, na makasha yao ya nguo yamewekwa nyuma ya gari. Na, mwajua, hilo ni jambo gumu.

8 Lakini Biblia ilisema juu ya watu kama hao, katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 11, “Hata ulimwengu haustahili kuwa na watu kama hao.” Na—nasema hilo kwa kuwa ninalimaanisha moyoni mwangu.

9 Na wengi wako hapa New Albany na Louisville, na huku karibu, huko chini Kentucky, na mahali mbalimbali ambapo si mbali sana, lakini hata hivyo hao ni waaminifu kuja, kuendesha magari kwenye barafu, theluji, chochote kile, wapate kufika hapa.

10 Sasa, Jumapili ijayo ni mkesha wa Krismasi. Nami nilidhani ya kwamba nilikuwa . . . nilikuwa na ujumbe wa Krismasi kwa ajili ya kanisa, ila ni—niliwahurumia sana hao jamaa wadogo, sina budi kusema kama wangeninii . . . kama ningekuwa hapa, basi hao jamaa wadogo labda wangeninii, wengi wao wakiwa mbali, wangekosa Krismasi yao na kadhalika. Kwa hiyo kwa namna fulani ingekuwa ni vigumu kwa jamaa hao wadogo. Lakini kabla ya kwenda . . . Sasa, sisi . . .

11 Ninajua ya kwamba sisi watu hapa hatuwafundishi watoto wetu hadithi za uwongo kama za Baba Krismasi. Hatuamini katika kumwambia mtu yeyote uongo, kwa hiyo hamtawadaganya watoto wenu. Upuuzi kama huo, hicho ni hadithi ya uwongo katika upeo wake, kwa kitu kama hicho kupachukua mahali pa Kristo katika Krismasi.

12 Na Krismasi imepoteza . . . Krismasi si ibada tena; ni sherehe, kunywa, kucheza karata, karamu za ulevi, ukafiri mtupu tu. Na sio . . . Nami nilitaka kuninii . . . Labda baada ya Krismasi nitazungumza tena juu ya *Krismasi*, mnaona, kusudi isije ikawanyima watoto . . . Lakini huwezi kusema hilo kwa watoto wadogo jinsi hiyo. Hao huwaona jamaa wadogo usiku wa Krismasi wakipokea zawadi za Krismasi na kadhalika namna hiyo, hawalielewi. Mnaona? Wananinii tu . . . hao ni wadogo sana. Na inatupasa kuwakumbuka, kwamba wao . . . kwamba wana

mambo shirika. Inatupasa kujishusha tupate kuwakumbuka hao jamaa wadogo, ya kwamba wao wenyewe . . .

13 Je! nimefungua sauti ku—kupita kiasi, ndugu, sauti kubwa mno kwake? Je! mwaweza kunisikia vizuri huko nyuma, nyuma kabisa? En-he? Hebu, ninasimama karibu mno. Ni maikrofoni gani inayofanya kazi, zote mbili, hii na hii? Na—nafikiri ni ile pale ndiyo nzuri. Hiyo ni—hiyo ni . . . Sasa, na hivyo je, hivyo ni bora zaidi? Sasa sawa, vema.

14 Sasa, jamaa hawa wadogo hawana budi kuelewa. Mwajua, wao ni—wao ni jamaa wadogo, nasi hatuna budi kukumbuka tulikuwa jamaa wadogo wakati mmoja, pia.

15 Nami nakumbuka wakati tulipokuwa watoto wadogo, wangeondoka na kukata maskini kichaka cha seda mahali fulani, naye mama angetengeneza bisi na kuzifungilia humo. Hayo ndiyo yote yaliyokuwako kwenye mti huo. Lakini hizo soksi ndogo, zilizochakaa zilining'inizwa hapo juu kama tu . . . Na, loo, na labda angechukua . . . labda mfuko mmoja wa peremende, na hizo peremende ndogo ngumu, (na mbili ama tatu kwangu, na mbili ama tatu kwa Humpy, na mbili ama tatu kwa *huyu*), vipande vidogo tu vya peremende, nasi tungeziweka hizo siku nzima, tukizimumunya hizo, mwajua. Na kuzifunga kwa kipande kidogo cha karatasi na kuziweka mfukoni mwetu. Na kama tulipata kifuniko kidogo cha siku nyingi cha bunduki, ama—ama vuvuzela ndogo ya kupulizia, lilikuwa ni jambo kubwa, lilituchangamsha.

16 Leo hii, hakika, ni tofauti. Walio maskini wamepata fedha kidogo na imefikia ambapo wanaweza kuwanunulia watoto wao vitu vingi zaidi, wanavalia vizuri zaidi, wanakula vizuri zaidi, wanaishi vizuri zaidi. Na kote—kote huku, nafikiri wao wana mazingira bora zaidi, na chini ya hali ya mshahara siku hizi. Na kwa hiyo, watoto wadogo, inakubidi kuwaacha wapate kitu.

17 Lakini daima mwe na hakika ya jambo hili, waambieni hakuna kitu kama Baba Krismasi, maana si sahihi. Moja ya siku hizi wataamka na kusema, "Vipi kuhusu Yesu, basi?" Mnaona? Mnaona? Kwa hiyo waambieni Ukweli, iweni wa kweli na kila mtu. Mwe Kweli. Na, hasa, msingewaambia watoto wenu kitu cha uongo, maana watasimama na kusema . . . Wanakuamini kuwa ni Mkristo, na wanakutaka uninii . . . Wanaamini ya kwamba unayowaambia ni Kweli. Kwa hiyo hakikisheni mmewaambia Ukweli, ndipo itatokea vizuri.

18 Sasa, na halafu ninataka kuwa na angalau usiku mmoja zaidi kama nikiweza, ama siku, kwa maskani, kabla sijaondoka kwenye miaka yangu ijayo ya huduma . . . mwaka wa huduma, hasa.

19 Na yakiwa ni mapenzi ya Mungu, ninataka kujaribu kufanya mikutano mingi ya nchi za ng'ambo mwaka huu, kwa kuwa ninahisi haja yake. Hasa sana huko Uswi- . . . katika Uswidi

na Norwe, na nyingi za Skandinavia—nchi za Skandinavia, na kushuka katika Asia. Najisikia ya kwamba inatupasa tuingie katika kilindi cha maombi juu ya mambo haya, tupate kujifunza njia za Roho Mtakatifu na jinsi ambavyo angetuongoza, na mambo ambayo tungepaswa kufanya.

20 Katika kusoma kwenye historia ya mwanzoni ya kanisa, iliyoandikwa na Broadbent, na Hazeltine, na mengi ya maelezo yao juu yake, *Wazee wa Nikea*. . . Na jana nilimaliza tu na maisha kamili ya Mtakatifu Martin ambaye kanisa Katoliki lilikataa kumfanya mtakatifu; Mungu alifanya hilo. Kwa hiyo wao. . . juu ya maisha yake makuu, na jinsi ambavyo ishara zile zile na maajabu zilimfuata mtu huyo moja kwa moja kupitia maisha yake; jinsi alivyowafufua watu wawili waliokufa, akatoa pepo wachafu, akanena kwa lugha zisizojulikana, na akaona maono na kadhalika, na ni mtu mashuhuri jinsi gani. Lakini, hata hivyo, na siri yenyewe ya uweza wake ilikuwa katika unyenyekevu mbele za Mungu. Nasi tunaona siku hizi ya kwamba kanisa, ingawa linafundisha uweza wake na kufundisha ishara kumfuata mwaminio, hata hivyo tunawaona wakiwa na kiburi, "mkuu mie, mdogo wee," na kwamba, sio—sio kama ilivyokuwa katika Kanisa la mwanzoni, mnaona. Walikuwa ni wanyenyekevu, na wakarimu mmoja kwa mwingine, na wa kupendeza, wenye huruma. Na ni tofauti sana siku hizi. Nami nashangaa kama mengi ya haya hayajatupotosha kutoka kwenye—kwenye kiini hasa cha—cha Ujumbe, hata, tunataka kujinyenyekeza. Jiwekeni. . . Kadiri unavyoweza kuwa mnyenyekevu zaidi, ndivyo Mungu atakavyokutumia vizuri zaidi.

21 Nikisoma juu ya hadithi za kubuni na hadithi hizi zote za uwongo, Krismasi yenyewe ni hadithi ya uwongo. Si ninii. . . Hakuna kitu cha halisi kuhusu Krismasi. Krismasi hata haikutajwa katika Biblia, kamwe hawakuiabudu siku ya kuzaliwa kwa Kristo. Hakukuwako na kitu kama hicho. Hilo ni fundisho la sharti la Katoliki ya Kirumi wala si fundisho la Kikristo, hakuna Maandiko kwake mahali popote katika Biblia na kwa miaka mia moja ya kwanza baada ya Biblia, unaona, hakuna lolote kuhusu hilo. Ni hadithi tu ya kubuni. Baba Krismasi, biashara, kila kitu, kitu hicho chote kimefungamanishwa katika upuuzi mtupu.

22 Kama ukirudi nyuma na kusoma mwanzo wake na kuangalia chini sasa, ungeona mahali tulipokuwa. Hakuna kitu kilichosalia, hakuna kitu kinachoweza kusaidia ila Kuja kwa Bwana. Hivyo tu. Hakuna kitu sasa kinachoweza kutusaidia kutoka kwenye machafuko haya ila Kuja kwa Bwana.

23 Hii ndiyo ile swichi ndogo inayodhibiti hizo kanda? Labda ni afadhali niyakague haya yote, nisiyasambaze tu, kwa maana ni fidhuli sana. Lakini ninasema hili kusudi. . . Je! kanda zinarekodiwa sasa? Msiziuze kanda hizi, mnaona, kanda hizi

si za kuuzwa. Zinaweza kusambazwa kanisani, ama vyovyote vile, lakini. . .maana ni. . .itasababisha machafuko, kweli kabisa. Mnaona? Kwa hiyo ishikilieni tu mpaka tutakapoiweka vinginevyo.

24 Sasa, kabla hutajauendea ujumbe, na kila mtu ajaribu kuwa makini na kutulia mwezavyo. Sitachukua muda mrefu sana, bali ninataka kuchukua wakati wangu kusudi. . .kulishindilia, kusudi mpate kuliona kweli. Sasa, hebu kwanza. . .Sasa, kama kila kitu kimewekwa kando, ninaamini, kufikia sasa kuna ninii. . .

25 [Ndugu Neville anasema viti vipo—Mh.] Naam, hebu hao mama wanaosimama upande huo hapo waje humu ndani. Kuna mahali hapa juu kwa ajili yenu dada. Naam. Hiki hapa kimoja papa hapa mbele. Hiki hapa kiti papa hapa nyuma. Kuna watoto hapa juu madhabahuni, kama mtu fulani anataka kuja humu na mtoto mdogo, na kumpa mtu fulani kiti chao, mtu mzima aliyesimama. Mbona, ipo nafasi kwenye—kwenye madhabahu papa hapa kwa ajili ya watoto, ndipo mtu mzima angeweza kupata kiti. Hao mama wanaosimama nyuma ya nguzo chomozi pale. Kama wewe. . .Ni huku nyuma kabisa pembeni, lakini ni. . .inashinda kusimama hapo juu. Kama ungetaka kusimama. . .

26 Hivi hapa vingine jukwaani. Sasa, baadhi yenu ndugu ambao mngetaka kupanda huku, watoto hawa wameninii. . . Huyu hapa mmoja ameketi hapa karibu na Ndugu Way. Njoni huku sasa, chukueni viti vyenu moja kwa moja hapa karibu, kusudi kila mtu. . .mnaweza kujisikia nyumbani kabisa, mjisikie mnaninii. . .jifanyeni kujisikia nyumbani kabisa. Hii hapa nafasi papa hapa, Ndugu Shelby, hapa juu papa hapa jukwaani, kama ukitaka kupanda kuja huku na kuketi karibu na sisi, papa hapa juu. Na Ndugu Evans na Ndugu Charlie, na ninyi, hiki—hiki hapa kiti papa hapa, na kimoja papa hapa, na viwili—viwili papa hapa. Panda moja kwa moja huku, ndugu hapo kutoka. . .njoo tu huku, mjistareheshe kusudi tuweze. . . kumfanya kila mtu atulie tu jinsi awezavyo kwa ajili—kwa ajili ya ibada, kusudi msichoke na kudhoofika na kusimama.

27 Baadhi yenu ndugu huko nyuma. . .dada huko nyuma kabisa kwenye ukumbi kule, mnaosimama huko nyuma kabisa ukumbini. Mnaninii. . .kungali kuna nafasi. Hii hapa nyingine, ni stuli ya piano inayoweza kutumiwa na mtu fulani, kama wangetaka kuja na kuketi juu yake. Ingekuwa ni sawa. Ninamwona mama mmoja pale nyuma anayeashiria kiti kilicho tupu karibu naye, kwa hiyo basi hiyo ni sawa. Jipeni tu starehe mwezavyo sasa.

28 Na sasa wakati tukijipanga, hebu. . .Ni kama saa nne na dakika ishirini, ishirini na tatu, kwenye siku hii ya kumi na saba ya Desemba. Inanyesha huko nje, hapa Jeffersonville asubuhi ya

leo. Na—na tuko vibaya kwa nje; bali tunajisikia vizuri ndani, vizuri sana, tukijua ya kwamba tunakaribia, Kuja kwa Bwana kumekaribia, na tunakaribia Umilele. Nasi tunamshukuru sana Mungu kwamba tunaweza asubuhi ya leo kusimama na kumpa mwaminio, na asiyeamini, Neno la Mungu aliye hai. Tukitumaini ya kwamba itakuwa ni siku kuu kwetu sisi sote kuyafahamu mambo ya Bwana.

29 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu kwa ajili ya maombi. Na wakati tumeinamisha vichwa vyetu, kama kuna yeyote angetaka kukumbukwa, mwinulie tu Mungu mikono yako, kumbuka ombi lako moyoni mwako. Asante.

30 Baba yetu wa Mbinguni, kwa kuwa sasa tuko kwenye maskani, sote tumeketi, na maikrofoni inafanya kazi, na vinasasauti vinarekodi, nao Wakristo wanaomba, maombi yanafanywa yajulikane. Na kwa majuma mawili au matatu mfululizo nimesoma siku zote kwa ajili ya ujumbe huu wa leo. Maneno machache tu ambayo labda Roho Mtakatifu angetumia kushindilia somo hili ndani ya mioyo ya watu, ili waweze kuona wakati tunaoishi, na wajiandae kukutana na Bwana Mungu. Tungewaombea wagonjwa wetu wote na wanaoteseka kila mahali.

31 Ee Yesu, likumbuke Kanisa Lako, Kanisa la ulimwenguni kote, kote ulimwenguni asubuhi ya leo, wengine huko nje mwituni, wengine chini kwenye bonde la kukata kauli, wengine wao wako kwenye kilele cha mlima. Na kote ulimwenguni watoto Wako wanakutegemea Wewe na kukuita Wewe. Na kama vile Yohana wa kale, kutoka kwenye Kisiwa cha Patimo, alivyosema, "Hata hivyo, na uje, Bwana Yesu."

32 Nasi tunatambua ya kwamba hatukosi uwepo wa adui, yeye daima yuko karibu apate kutuzuia na kutusimamisha, na kufanya lolote awezalo. Lakini, Ee Bwana, wape watoto Wako imani asubuhi ya leo, nguvu za kuinuka juu kushinda adui, kuifungua mioyo yao na kuzifanya nafsi zao shamba la ardhi yenye rotuba ambapo Neno la Uzima linaweza kupandwa, na kusababisha furaha tele na mavuno mengi mno.

33 Ninaomba, Bwana, kwamba utalibariki Neno Lako na watumishi Wako. Isaidie hii sauti yangu dhaifu nipate kuwa imara kwa upako wa Roho Mtakatifu. Halafu basi kwenye mstari wa maombi, tupe nguvu na imani, Bwana, kusudi kusiwe na mtu mnyonge miongoni mwetu tutakapoondoka kwenye jengo hili. Tujalie, Bwana.

34 Tunajua ya kwamba tunaishi katika wakati wa mwisho. Nasi tunakuomba utubariki sasa tunapoendelea kukungojea na kulisoma Neno Lako. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

35 Sasa nitasoma sehemu mbili ama tatu katika Maandiko, na kama nilivyotangaza Jumapili iliyopita ya kwamba leo hii nitajaribu kuzungumza juu ya: *Ukristo Dhidi Ya Uabudu*

*Sanamu*. Na hilo ndilo somo letu la asubuhi ya leo. Na, sasa, mimi si mwanatheolojia, si mwanafunzi wa Biblia hata kidogo, ni mtu tu asiye na elimu ninayempenda Bwana Yesu kwa moyo wangu wote. Mimi sidai kuwa mwanatheolojia wala kujaribu kupachukua mahali pa mmoja, bali ni kujaribu tu katika unyenyekevu wa moyo wangu kueleza mambo hayo ambayo najisikia Roho Mtakatifu amenifunulia, nami sina budi kuyatoa kwa kanisa langu. Kwa kuwa ni shauku yangu kwamba kanisa hili likue, kwamba kanisa hili liwe sawa kiroho. Ni matakwa yangu kwa sababu kanisa hili ni matakwa ya Mungu, na matakwa Yake ni matakwa yangu. Kwa hiyo sina budi kulishughulikia jambo hili.

36 Huku nikisoma kwa wanahistoria wa mwanzoni, juu ya Ireneo na hao wengine, jinsi walivyoliweka kanisa lao bila kunajisiwa na mambo ya ulimwengu, jinsi ambavyo hao waalimu wa kale walivyoinuka kule na kudumu na hiyo Injili kwelikweli. Biblia wakati huo haikuwa imeandikwa katika muundo tulio nao sasa, si mpaka kwenye yale Matengenezo, naye Luther akaichapisha. Lakini wao—wao walikuwa na kile walichokiita *Injili na Mtume*. *Injili na Mtume*, nao walidumu na hicho.

37 Sasa, kwa ajili ya sehemu zetu mbili tunazokusudia kusoma asubuhi ya leo, moja ya hizo inapatikana katika Kitabu cha Yeremia, mlango wa 7, na kuanzia kifungu cha 10 hadi cha 18. Mahali pengine panapatikana katika Matendo 7:49. Na kama mnataka kutia alama fungu hilo kwa hili, ama somo linalotokana na hili, Yeremia 7, kingekuwa ni kifungu cha 18. Ninataka kuanza kusoma kutoka kifungu cha 10.

> *Kisha mtakuja na kusimama mbele zangu katika nyumba hii, iitwayo kwa jina langu, na kusema, Tumepona; ili mpate kufanya machukizo hayo yote?*
>
> *Je! Nyumba hii, iitwayo kwa jina langu, imekuwa pango la watu wanyang'anyi machoni penu? Angalieni, mimi, naam, mimi, nimeliona jambo hili, asema* Bwana.
>
> *Lakini enendeni sasa hata mahali pangu palipokuwapo katika Shilo, nilipolikalisha jina langu hapo kwanza, mkaone nilivyotenda kwa sababu ya uovu wa watu wangu Israeli.*
>
> *Na sasa, kwa sababu mmezifanya kazi hizi zote, asema* Bwana*, nami nikasema nanyi, nikiamka mapema na kunena, lakini hamkusikia;. . .nikawaita wala hamkuniitikia;*
>
> *Basi, nitafanya* hili *kwa nyumba hii, iitwayo kwa jina langu, mnayoitumainia, na mahali hapa nilipowapa ninyi na baba zenu; kama nilivyotenda Shilo.*

*. . .nitakuwa nimewatupa ninyi mbali na macho yangu, . . .nitawatupa ndugu zenu wote, nilivyowatupa ndugu zenu wote, yaani, wazao wote wa Efraimu.*

*Basi, wewe* usiwalipie *watu hawa, usiwaombee . . . watu hawa, wala usiwapazie sauti yako, wala* kuwaombea *dua, na wala usinisihi kwa ajili yao; kwa maana sitakusikiliza.*

*Je! Huoni jinsi wanavyotenda katika miji ya Yuda, na katika njia kuu za Yerusalemu?*

38 Sasa ninataka kusimama kabla sijasoma kifungu cha mwisho cha haya. Hebu nianze tena sasa. Mungu akiwakemea watu hawa, na kusema, "Hata usiwaombee." Hebu nianzie kwenye kifungu cha 16 na kusoma kupitia cha 18 sasa. Sikilizeni kwa makini.

*Basi, wewe usiwaombee watu hawa, wala usiwapazie sauti yako, wala usiwaombee dua, na wala* kunisihi *kwa ajili yao; kwa maana sitakusikiliza.*

*Je! Huoni . . .Huoni jinsi wanavyotenda katika* mji *wa Yuda, na katika njia kuu za Yerusalemu?*

*Watoto huokota kuni, . . .baba zao huwasha* mioto, *na wanawake hukanda unga, ili kumfanyizia mikate malkia wa mbinguni, na kuwamiminia miungu sadaka za kinywaji, wapate kunikasirisha mimi.*

39 Sasa, nataka kufungua sasa kwenye Kitabu cha Matendo, mlango wa 7, na kuanzia kifungu cha 44, na kusoma hadi cha 50.

*Ile hema ya ushahidi ilikuwa pamoja na baba zetu jangwani, kama alivyoagiza yeye aliyesema na Musa, ya kwamba aifanye sawasawa na mfano ule aliouona;*

*Ambayo baba zetu, kwa kupokezana, wakaiingiza pamoja na Yesu katika nchi ya Mataifa wale, ambao Mungu aliwafukuza mbele ya baba zetu, mpaka siku za Daudi;*

*Aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye aliomba ampatie Mungu wa Yakobo maskani.*

*Lakini Sulemani alimjengea nyumba.*

*Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono, kama vile asemavyo nabii,*

*Mbingu ni kiti changu cha enzi, na nchi ni pa kuwekewa miguu yangu; ni nyumba gani mtakayonijengea? Asema Bwana. Au ni mahali gani nitakapostarehe?*

40 Sasa, mnaweza kuona kwa kusomwa kwa Maandiko, ya kwamba, mahali ninapoliweka wazo langu asubuhi ya leo, juu ya "uabudu sanamu," kwanza, kwa kuanzia. Ni machache mno yaliyoandikwa juu ya *uabudu sanamu*. Hamna vitabu vingi vya

kuelezea uabudu sanamu, kwamba uabudu sanamu ni nini, na hata hivyo ulimwengu umejaa huo. Nafikiri sababu yake ni kwamba, ni kwa sababu kweli haujaelezewa kwa watu, hawajui ni kitu gani. Na yamekuwa ni majaliwa yangu, na majaliwa yangu makuu maishani mwangu, katika kusafiri, kuona baadhi ya ibada za sanamu, kujua ni nini.

41 Na basi katika kuchunguza uabudu sanamu, majuma machache yaliyopita, hadithi za kubuni, hadithi za kubuni za Wayunani na hadithi za kubuni za Warumi, ndipo inanirejesha nyuma kuona kama wanaua . . . wangali wanaendeleza jambo lile lile, kuona kama uabudu sanamu ungali kama ulivyokuwa hapo mwanzo. Siku hizi katika kusafiri, nikiona uabudu sanamu; halafu kuona jinsi ulivyoanza, nikisoma jinsi ulivyoanza huko nyuma kwenye . . . katika siku za mwanzoni; ninaona ya kwamba haujabadilika.

42 Sasa, nimekuwa India, India imejaa uabudu sanamu. Wana watembea motoni kule na wengine . . . Nafikiri, alasiri moja nilipofika Bombay, nilitumbuizwa alasiri hiyo na . . . Mimi . . . mtu fulani aliniambia, nisingeweza kuwatofautisha, walikuwa tu kwenye hekalu la Jaini. Na zilikuwa ama ni kumi na saba ama saba, dini mbalimbali, nami nina hakika sana zilikuwa ni dini kumi na saba mbalimbali zilizokuwa zimekutana nami pale kulipa Neno changamoto, na kila moja ya hizo inampinga Kristo kwa dhati. Dini kumi na saba mbalimbali! Nazo zilikuwa . . . Walitufanya tuvue viatu vyetu hekaluni, na kuingia, na wakatuketisha kwenye mito. Na ingechukua muda kupitia kwenye mapayo yote (kama ninavyoyaita) yaliyotupasa kupitia. Lakini meya wa mji alituingiza mle, mwenyewe akiwa ni Mhindu, ambayo ni Mwislamu.

43 Naye Mohamad alikuwa ni nabii, naye alitokana na ukoo wa Ishmaeli ambaye pia alikuwa ni mwana wa Ibrahimu.

44 Na ulikuwa ni ukoo huu ambao mwinjilisti huyu mashuhuri ulimwenguni siku hizi, ambaye, alimkimbia mmoja wa watu wao ambaye alimpa changamoto ya shindano la kuamua katika Neno. Na, kwa maoni yangu, mwinjilisti huyo alipaswa kusema, "Sina karama za uponyaji, bali mwili wetu wa waaminio unazo. Naomba unipe saa chache, nami nitamleta mtu fulani hapa." Mnaona? Lakini, bila shaka, katika kufanya hilo, basi mwinjilisti huyo angalijianika kwa madhehebu yaliyokuwa yakimdhamini, na ndipo angetupwa nje.

45 Na kisha juu ya wazo la pili la jambo hilo, siamini ningalimwacha huyo asiyeamini kupata ushindi juu ya Neno la Mungu. Kama ningalishindwa, ningali ningalisimama pale na kuonyesha imani yangu na tumaini langu kwa Mungu kwamba Yeye anabaki yule yule. Kama vile wale wana wa Kiebrania walivyosema, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na tanuru hii ya moto, lakini hata hivyo hatutazisujudu sanamu zako." Naam,

ninaamini lingalikuwa jambo la kishujaa zaidi. Halafu basi tena ningeninii . . .

46 Kwa kuwa alikuwa ni daktari wa theolojia na anayafahamu sana Maandiko, jinsi alivyo mwinjilisti mashuhuri, na ni mtu mwenye nguvu, ninaamini ya kwamba ningalimpa changamoto kwenye Neno, kama Yesu alikuwa Ndiye Kristo ama siye, ama kama Mohammad alikuwa ni nabii, na alikuwa amemthibitisha kwa Biblia yake mwenyewe. Kama huo ungekuwa ni wito wangu (katika Biblia) kama vile ulivyo kwa mwinjilisti huyo, kulielezea, ningalichukua msimamo huo badala ya kutoroka na kurudi nyuma. Hiyo ilionyesha . . . Hilo halionyeshi ujasiri kamili wa Mkristo ambaye atasimama hapo, aishi au afe. Mungu anaweza kukomboa. Ninaamini ningaliomba usaidizi wake juu ya jambo hilo.

47 Lakini wanasahau kuwazia juu ya Bombay wakati yule kipofu kule, hao Waislamu, usiku huo alifunguliwa macho mkutanoni. Wasingetaja hilo.

48 Lakini, hata hivyo, kuhusu watu hawa, hao si wanafiki. Ni watu waaminifu, waaminifu tu kama wewe na mimi, na wakati mwingine zaidi ya vile tulivyo hapa Marekani. Hao si wanafiki. Wanaamini hilo kweli na kulitekeleza kwa yote yaliyo ndani yao.

49 Hebu niwape jambo dogo juu ya uabudu sanamu. Ninasahau jina la mungu ambaye ni mungu wa hao watembea motoni, bali ni sanamu kubwa mno ikiwa na ninii nene mno, kubwa . . . kitu kinachofanana na uso wa mwanadamu, kitu kama taswira ya uso, ikiwa na masikio makubwa mno, manene kusikia dhambi zao zote na kadhalika. Na rubi kubwa mno kama herini katika ninii yao . . . masikioni mwake hapa, ambazo, labda zingegharimu nusu milioni kila moja, labda; hilo huenda likawa ni kadirio la juu sana, huenda ni kadirio la chini sana. Lakini, loo, vito vyenye thamani kubwa mno kwenye sanamu hii!

50 Naye kuhani wa hekalu hilo humleta mkulima maskini, haimbidi kuwa . . . wa kawaida tu, si lazima awe ni mtu maalum. Ni mtu wa kawaida tu, mkulima anayetaka kutoa shukrani kwa mungu wake kwa ajili ya mazao mema. Na, katika kufanya hilo, anaonyesha imani yake katika mungu wakati akija hekaluni na kubarikiwa na kuhani wake.

51 Na halafu kuninii . . . akijiandaa kutembea kupitia kwenye dimbwi la makaa ambalo lina kina cha futi nyingi na upana wa futi nyingi, nalo limepuliziwa kwa viyoyozi likawa jeupe kwa moto. Sasa, hiyo si kujifanya, ni kweli. Yeye anaenda mbele za sanamu hiyo, anakiri dhambi zake kwa kuhani huyu, nao wanammwagilia maji; maji matakatifu, na kadhalika, ambayo kuhani amebariki.

52 Halafu basi, mara nyingi, wanachukua kulabu, ndoana, nene, kubwa, labda ina upana wa nusu inchi hadi theluthi tatu ki—kipenyo, kipenyo kutoka n—nchani mpaka upande wa

nyuma ya kulabu hiyo. Nao wanaweka mpira mdogo wa maji kwenye hiyo, kama maskini pambo dogo la mti wa Krismasi, na mpira mdogo, na kuujaza maji upate kuwa mzito. Nao wanachukua, hasa, maelfu ya kulabu hizo na kuzitia mwilini mwao, wakizing'oa. Wakati zikiingia ndani, mwilini mwao, wanazing'oa, wapate kupitia kwenye mateso ili kumfurahisha mungu wao, sanamu hiyo. Hao si wanafiki.

53 Halafu, mara nyingi, wanatoa ulimi wao na kuchukua fumo yenye uma, kuuchoma ulimi wao na kupitia pua yao na kushikanisha pamoja, wanachukua mishono ya uzi na kuushona mdomo wao pamoja kama kuna ninii . . . walisema uongo. Na mateso kama hayo!

54 Na kisha wanaketi chini karibu na dimbwi hili kubwa la moto. Wanamchinja mbuzi, kuiridhisha sanamu hiyo, kutoa uhai kwa ajili ya dhambi zao. Nanyi mnapaswa kusikia m—mngurumo wakati mbuzi huyo anapochinjwa. Wanakiri dhambi zao juu yake na kumchinja huyo mbuzi, wakitupa ninii . . . wakichukua hiyo damu kama upatanisho.

55 Halafu basi kama huyu mtembea motoni, kama akiogopa na kukimbia humo motoni, anajiletea aibu. Bali inambidi kutembea polepole na kwa utaratibu kwenye makaa haya ya moto. Na wakati mwingine yana kina cha futi kumi na tano, makaa haya ya moto. Na labda futi kumi na tano labda kina cha futi kumi na tano na labda urefu wa yadi thelathini ama yadi arobaini, na yapata, loo, labda upana wa futi nane ama kumi. Nayo ni meupe kwa moto. Naye hajavaa kitu ila kitambaa, ambacho ni kitambaa kidogo cha kiunoni alichojizungushia kiunoni mwake. Naye anatoka anaenda huko nje, huku amejining'inizia hizi zote, na kutokwa damu, na ndoana za samaki na chochote mwilini mwake nwote, anajitia kichaa mpaka udenda mweupe unachuruzika kutoka kinywani mwake.

56 Naye huyu hapa anakuja, akitembea kupitia moto huo, na anavuka upande wa pili, pasipo kudhurika hata kidogo, kupitia motoni, na labda miguu yake inazama kwa kina *hiki* (miguu) kuingia ndani ya moto, futi mbili au zaidi anapotembea, akiyakokota hayo makaa mekundu kwa moto kwa mwili wake wa kibinadamu, akitembea kupitia moto huo na kutokea upande wa pili pasipo kudhurika. Ungeweza kuangalia miguu yake, hamna mkwaruzo wala mchomo.

57 Na katika kuangalia hivyo, na kuwazia, kama dhabihu kwa sanamu ya kipagani, kwa damu ya mbuzi, kwa imani katika kitu kama hicho ingeweza kumwokoa kafiri na moto, Damu ya Yesu Kristo ingemfanyia nini mwaminio wa Mungu aliye hai?

58 Sasa, uabudu sanamu ni kitu cha kigeni. Kote katika nyakati tumekuwa nao, tangu ninii . . . nadhani, mwanzo wa wakati. Sasa, utaratibu wa uabudu sanamu ni mtu ambaye huisimamisha sanamu hii, anaitengeneza sanamu hii, kisha

anaingia na kujiandaa kwa ajili ya ibada hii kuu. Sasa, yeye anaamini ya kwamba sanamu hii imefanywa katika sura ya mungu fulani ambaye kamwe yeye. . . hajapata kumwona. Hana umbo, kwa hiyo yeye anaamini yuko katika sura ya sanamu hii anayomfanyia huyu mungu.

59 Sasa, msiache hilo liwaache! Hiyo "sanamu" iko katika sura ya mungu wa kujibunia ambaye anaamini huyo ndiye.

60 Halafu anaenda mbele ya sanamu hii na kusujudia mwenyewe, na kuamini kuwa mungu asiyeonekana anashuka na kuingia ndani ya sanamu hii, na anaamini kwamba anazungumza na mungu kupitia sanamu hii, kwamba mungu anajileta mwenyewe ndani ya sanamu hii na kumjibu. Na wengi wenu nyinyi waalimu hapa ambao mmesomea hadithi za kubuni. . . Hata miungu hao, walifanya vita mmoja kwa mwingine, walivyodai, na kila kitu, katika siku hizo.

61 Sasa, kwa maneno mengine, mungu huyo anajiponozi kutoka kwenye msimamo wake wa kimiujiza, akaingia kwenye sanamu hii, naye anamjibu mwabuduo kupitia kwenye sanamu hii. Naye mwabuduo, katika namna fulani ya hisi ya mhemko wa kujichochea, anaamini ya kwamba sanamu hiyo inazungumza naye, moyoni mwake, naye anasamehewa dhambi zake na kadhalika, kupitia sanamu hii, ambalo kwa udhahiri linaonyesha ya kwamba ni ibilisi. Ibilisi ndiye anayefanya hilo.

62 Nao hawafanyi mambo vivi hivi tu; baadhi yao hufanya, bali kuna waabuduo wa kweli hasa wa vitu hivyo. Kwa mfano, ningeweza kuwasimulia hadithi za jinsi hao mapepo kwenye sanamu hizo walivyofanya kila namna ya mambo, kufanya damu itoke kwenye vitu, na chochote kile. Hao—hao ni—hao ni pepo!

63 Na endapo huamini katika. . . kweli pepo yupo, huamini Mungu yupo. Hakika, inakubidi kuamini vinginevyo, ubaya na uzuri. Kwa hiyo kuna pepo halisi, naye ni mtu. Sio *wazo*, yeye ni *mtu*.

64 Sasa, yapo mafundisho yanayoendelea yanayosema, "Ibilisi ni—ni wazo baya tu unalopata." La, la, sivyo. Ibilisi ni mtu.

65 Watu hao hao wanaamini ya kwamba "Roho Mtakatifu ni—ni wazo zuri tu unalopata." Lakini msiamini hilo. Roho Mtakatifu ni Mtu, ni Utu wa Kristo katika umbo la Roho.

66 Sasa, hawa waabudu sanamu. . . (Nawe umeandaa Maandiko yako ama nafasi ya Maandiko yako. Hu—huenda nikarejea kwa baadhi yake katika muda mfupi, Maandiko, huenda tukasoma baadhi yake.) Sasa, hawa waabudu sanamu, wakisujudu mbele ya sanamu, wanaamini ya kwamba mungu wanayemwabudu amewakilishwa katika sanamu hii. Sasa, mmelipata hilo, ya kwamba huyo mwabuduo si mnafiki? Yeye kwa kweli anawasiliana na kitu fulani kilicho ndani ya sanamu hiyo, kwa kuwa kinamrudia, anafanya jambo fulani; analipata

kutoka kwa sanamu hiyo, ambayo ni mungu wa kubuni, si Yule wa kweli.

67 Na mara nyingi ibilisi huingia katika vitu hivyo. Pia ibilisi huingia mikutanoni wakati mwingine na kujifanya kama Mungu. Nimeona jambo hili katika huduma yangu.

68 Sasa, kumbukeni, hii ni ninii tu. . .tunafundisha tu asubuhi ya leo. Nami ninalitaka kanisa hili, wakati nitakapoondoka humu kwenda nje hudumani, ninawatakeni mkae na mchungaji wenu na mdumu na Mafundisho ambayo yamefundishwa hapa. Dumuni na Neno hili, msiliache! Dumuni moja kwa moja na Neno hata iweje, dumuni na Neno hilo! Mnaona? Sasa, na kwa sababu tu ati ninaondoka. . .Mimi ni mmoja tu wa wachungaji hapa. Ndugu Neville hufundisha jambo lile lile ninalofundisha, kwa hiyo njoni moja kwa moja kanisani mkalisikilize Neno.

69 Sijui Yeye ataniongoza wapi. Nilimwambia mke wangu asubuhi ya leo mezani, "Kuna kitu ndani yangu ambacho kimelia miaka hii yote, ninaenda kutafuta kujua ni kitu gani." Sasa, sijui kitaongoza njia gani, kitakapoenda, bali aniongozako nitafuata.

70 Sasa, uabudu sanamu, ungaliko siku hizi. Tunaona. . . Ninawaona watu wakija madhabahuni, pamoja na misemo mipofu ya waalimu vipofu, ambao watasema, "Jiweke tu wazi, sahau kila kitu, fanya akili yako tupu. Utakuwa Eliya. Utakuwa *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*." Ni uongo wa jinsi gani! Humjii Mungu. . .Hiyo ni kuifungulia nafsi yako kila namna ya pepo wa ibilisi kuingia. Usifanye hivyo. Huna budi kukumbuka kuna pepo, naye humwiga Kristo kabisa, karibu kikamilifu.

71 Nilikuwa nikisoma kwenye *Maisha ya Mtakatifu Martin* wakati fulani uliopita, ambapo mvulana, kwa kweli alikuwa ni mtawa, naye akasema ya kwamba Mungu alikuwa amemwita apate kuwa mmoja wa manabii wa kale, "Nisikilizeni mimi, mimi ni mmoja wa manabii wa kale." Na shule. . .Martin, bila shaka, asingesikiliza kitu kama hicho. Kwa hiyo wao hawakuamini hilo kwa kuwa maisha ya mvulana huyo hayakulingana nalo. Hatimaye akasema, "Nitawathibitishia ya kwamba nimeitwa kuwa nabii wa kale. Jamaa mdogo tu," kasema, "bali nimeitwa."

72 Mnaona, "Karama na miito havina majuto." Mnaona, wanaliacha Neno, na unapoliacha Neno unaingia katika chochote kile.

73 Ndipo mvulana huyu akasema, "Usiku wa leo, yapata usiku wa manane, Mungu atanipa joho jeupe, nikae miongoni mwenu nyote nalo, kuonyesha ya kwamba mimi ni nabii wa kale." Kwa hiyo wao. . .usiku huo wote wakasikiliza, na kunong'ona, "karibu," na watu wakisafiri. Ndipo mvulana huyo akapata joho jeupe. Wakati mgeni alipoondoka, walienda wakaliangalia hilo joho, lilikuwa ni vazi jeupe, la kweli, halisi, lilionekana ni zuri sana.

74 Lakini, maskini yule askofu, asingelipata hilo kamwe. Halikuonekana ni sawa, kwa maana, halikuambatana kabisa na Maandiko (joho jeupe).

75 Basi alipofanya hivyo, wao walisema, "Hebu ulichukue joho hili uende ukasimame mbele ya Mtakatifu Martin, yule mtu wa Mungu." Naye asingefanya hivyo. Asingesimama mbele ya huyo nabii wa kweli. Asingesimama; nao wakamlazimisha kufanya hivyo. Na walipoanza kumpeleka, hilo joho likatoweka likaenda mahali fulani, hawakujua mahali lilipokwenda. Mnaona, inapofikia kwenye shindano la kuamua!

76 Kama una dhahabu halisi haikubidi kuwa na wasiwasi kama ni nzuri ama si nzuri, itastahimili jaribio mahali popote. Na Roho halisi wa Mungu atastahimili jaribio kwa kuwa amejaribiwa kwenye Neno la Mungu. "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu."

77 Nimewaona watu wakiingia katika mipagao, watu wazuri. (Sasa mnaweza kuona ni kwa nini sitaki ka—kanda hii iuzwe.) Nimeona watu wazuri, na Wapentekoste, wachungaji ambao hawakuelewa, watu wanaingia katika mpagao na kupagawa, na kila kitu namna hiyo, na—na kufanya mambo, na hatimaye wanaishia kwenye hospitali za wendawazimu. Ilikuwa ni kuifungua mioyo yao, watu wasio na hatia, ndipo pepo wakaingia na likatendeka. Huyo hapo pepo halisi!

78 Nilikuwa nikisoma hapa ambapo mmoja alimjia... Ninaamini ilikuwa ni Ireneo ama Martin, mmoja wao, (baadhi ya wanafunzi wa Biblia wenye ujuzi zaidi katika jambo hili kuliko mimi), alikuwa na taji ya dhahabu kichwani mwake, amevaa joho jeupe, viatu vilivyotiwa njumu ya dhahabu, na kusema, "Mimi ni Kristo, nikiri Mimi!" Mtakatifu huyo asingefanya hivyo. Huyo nabii halisi wa Mungu alisimama hapo, akangojea. Nao wakamwambia mara mbili ama tatu, "Mimi ni Kristo, nikiri Mimi!"

Akasema, "Kristo wetu haji namna hiyo."

79 Hiyo ni kweli, huna budi kulifahamu Neno! Dumu kwenye Neno! Unaona, vita vikuu vimewadia. Sasa, tumeiga kanisa kwa miaka na miaka, bali wakati umewadia sasa ambapo Yambre na Yane watashindana na Musa kama Biblia ilivyosema wangefanya. Na vitakuwa ni vita vya kiroho, mapambano. Kutakuwako na wengine watakaoendelea tu, kanisa la kimadhehebu litazidi kwenda tu moja kwa moja liingie katika utawala na liendelee jinsi linavyoendelea. Bali ninamaanisha mwaminio wa kweli anakuja kwenye uwanja huo wa vita, na afadhali uwe na maarifa na ujue unalofanya, la sivyo ungeweza kupokea pepo mchafu kwa urahisi sana na usijue. Kama ni kinyume na Neno hili, usiliamini! Dumu na hilo Neno!

80 Uabudu sanamu, uabudu sanamu ni wa kale, ni wa kale hapa Marekani. Na miaka mingi iliyopita, Wahindi wa Kipueblo,

na huko Arizona, walikuwa na uabudu sanamu. Na, hiyo ilikuwa, wa—walikuwa na mungu wa mvua. Naye huyo mungu wa mvua alikuwa. . . wanachukua ka—kasa wa matopeni, nao wakatengeneza sanamu ya kasa wa matopeni. Nao wakamtia madoadoa mwili mzima kana kwamba ametoka matopeni. Nao wangejitupa mbele ya huyu kasa wa matopeni, wakiamini kulikuwako na mungu wa mvua aliyeshuka akaingia ndani ya ganda la kasa huyu wa matopeni na kunena nao kupitia huyu kasa wa matopeni. Kwa kuwa waliamini ya kwamba ninii. . . aliishi katika matope na unyevu, naye alikuwa ni mungu juu yake. Walikuwa na. . . ni hadithi ya kubuni, ki—kiinimacho kwamba ni kweli.

81 Sasa, nao waliabudu ibilisi kwa kufanya hivyo. Kumwabudu kasa wa matopeni, wakidhania alikuwa ni mungu wa mvua, walijiletea pepo juu yao, hakika, maana waliifungua mioyo yao kwake. Bali ilikuwa ni roho chafu!

82 Watu wengi sana siku hizi wanaifungua mioyo yao kwa kitu kibaya! Unapata roho fulani kweli, bali mara nyingi analipinga Neno, akisema, "Siku za miujiza zimepita! Hakuna kitu kama *hiki* ama *kile*." Kumbukeni, huyo ni ibilisi akiiga Ukristo. Mungu na atusaidie tutakapolifikia hili baada ya kitambo kidogo, mpate kuliona, mnaona, kwamba ni pepo mchafu akiuiga Ukristo. Bali si Roho wa Kristo, kwa kuwa Roho wa Kristo huja kwenye Neno kila wakati. Yeye hawezi kulikana Neno Lake Mwenyewe.

83 Sasa, Ukristo ulipokuja Rumi, Rumi, katika jiji lenyewe la Rumi, kulikuwako na hekalu mia nne za kipagani ndani ya ukuta wa maili saba. Hekalu mia nne za kipagani, nazo zilikuwa ni za miungu wa kiume na wa kike. *Miungu wa kiume na miungu wa kike*, "wanawake na wanaume." Miungu, mia nne mbalimbali. Wazia hilo, mia nne!

84 Sasa, hayo ndiyo Paulo aliyakuta wakati alipokwenda Rumi. Hayo ndiyo Akila na Prisila walikutana nayo wakati walipotumwa kutoka Pentekoste na wakaanzisha kanisa huko Rumi; hayo ndiyo waliyokabiliana nayo, ibada za kipagani za sanamu. Kulikuwako na karibu watu milioni mbili huko Rumi, katika jiji kuu la Rumi; hiyo ni kusema, watumwa, na wakaaji wa vitongoji vya nje, na kadhalika, karibu watu milioni mbili. Lakini kuta zilizozunguka Rumi zilikuwa ni maili saba. Na ndani ya hizo maili saba, papo hapo chini ya mlima, kulikuwako na hekalu mia nne za kipagani, kwa miungu wa kiume na wa kike wa kipagani.

85 Sasa, ningetaka kuzungumza kidogo hapa juu ya jambo fulani ambalo nimetoa kwenye historia, nami nina moja papa hapa pamoja nami. Jinsi walivyoingia katika ibada, walikujaje kuabudu? Mpagani alikujaje kuabudu? Jambo la kwanza alilofanya lilikuwa ni kwenda hekaluni na kukutana na kuhani,

kuhani wa kipagani. Kisha angempa sadaka ya kiasi fulani cha fedha, na halafu atoe dhabihu, mnyama, kumtuliza mungu ambaye alitaka kuzungumza naye.

86 Na katika wakati mwingine, katika hekalu moja, kungekuwa na zaidi ya aina moja ya mungu. Kungekuwako na "miungu wa kiume, miungu wa kike," na chochote kile, katika hekalu moja.

87 Kwa hiyo kuhani wa kipagani. . . Angemwendea na kumpa kiasi fulani cha fedha, naye kuhani wa kipagani angempa mshumaa, mshumaa tu wa kawaida wa shahamu. Ndipo mwabuduo angeuchukua mshumaa huu, akiisha kumlipa kuhani, angeuchukua mshumaa huu na kwenda kwenye madhabahu fulani ya mungu huyu aliyetaka kuzungumza naye. Na juu ya madhabahu hii kulikuwako na moto, ambapo sadaka hiyo ingeteketezwa. Chini ya sanamu hii, hekalu kuu ya shaba, ama—ama sanamu, naye akaichukua hii heka-. . . mshumaa huu na kuuwasha kwa moto wa madhabahu, moto wa madhabahu ya sanamu hiyo, akauwasha mshumaa kisha akaenda chini ya ma—madhabahu mbele ya sa—sanamu, akauweka mshumaa huu chini. Halafu baada ya kuuweka mshumaa chini . . .

88 Nadhani ni ili kwamba mungu fulani miongoni mwa miungu wengine wote angejua ni sanamu ipi alipaswa kuiendea, mwajua, kurudi na kuzungumza naye. Kazi ya huo mshumaa, sijui. Lakini angeuweka mshumaa chini, uliowashwa na mioto ya madhabahu.

89 Na kisha angerudi sakafuni mwa maskani hiyo, na hapo ajilaze kifudifudi sakafuni. Na hapo angeiweka nafsi yake yote, nguvu zake zote katika maombi yake, na kumwomba mungu huyu mkuu wa aina fulani, mungu wa kiinimacho, wa kujibunia, amwombe mungu huyu ashuke katika sanamu hii na kunena naye.

90 Ilisemekana ya kwamba, "Mmoja wa wale wafalme wakuu angesujudu sana mbele ya sanamu ya Apolo hata kweli angeweza kusema alisikia sauti zikitoka kwenye heka-. . . kutoka kwenye—kutoka kwenye sanamu hiyo, ikimjibu." Akisujudu!

91 Ungesema sasa, "Ndugu Branham, je! alisikia sauti?" Sina tashwishi kwamba alisikia, bali ilikuwa ni sauti ya ibilisi. Hakukuwako na kitu kama Jupita, mungu, na miungu hawa wengine wote waliokuwa nao.

92 Lakini walisujudu, nao wakalala hapo na kuabudu, wakamwabudu mungu huyu wa kisiri ambaye hawakujua lolote kumhusu, wakati roho yake ilikuwa katika sanamu waliyodhani ilifanana naye. Walitengeneza sanamu yake, na hiyo ikakubalika kwake.

93 Ndipo wakatoa sadaka. Ndipo wakati alipojipagaza katika mhemko huu, alienda tena mbele ya sanamu hiyo na wakati huu kuhani huyo wa kipagani alikuwa amemletea cha—chakula na

kinywaji, na kuviweka miguuni pa sanamu hiyo. Na halafu... (Sasa, ninaninii...nimeliandika hapa kwenye ukurasa huu, ninalisoma moja kwa moja kutoka kwake. Mnaona?) Naye angeinama miguuni pa sanamu hii, na kuchukua baadhi ya sadaka hii ya kinywaji na kukionja, na kunyofoa chakula kidogo, kisha kukimwaga juu ya miguu ya sanamu hii.

94 Alikuwa akifanya nini? Kufanya ushirika na pepo; kushiriki na pepo, miungu wa kiume na wa kike. M—mfano tu wa Mkristo akifanya ushirika na Kristo, akila ushirika. Huo ulikuwa mfano ambao kanisa la kwanza ama wasafiri wa kwanza wa Injili (waliokuja Rumi) walikuta, ilikuwa ndani ya watu hawa katika ibada za namna hii.

95 Baali alikuwa ndiye mungu mwenye sifa sana wa wakati huo wote, miongoni mwa sanamu, alikuwa ni Baali (B, a maradufu, l, i), yeye alikuwa mungu-jua. Halafu alikuwa na m—mke, mungu-mwezi, mungu wa kike, Ishta, I-s-h-t-a, Ishta. Na pia linatamkwa A-s-t-a-r-t-e, "Astarte." Yuko kwenye sarafu ya Kirumi. Aliitwa mungu mke, mungu-mwezi wa kike, ama "malkia wa mbinguni, mama wa miungu," mungu-mwezi. Naye mungu-jua alikuwa Baalim.

96 Vema, karibu wapagani wote waliliabudu hilo jua. Hata Wahindi walikuwa wakifanya jambo lile lile wakati—wakati tulipokuja, tulipoianzisha Marekani hapa, wakati Marekani ilipoanzishwa. Walikuja, baba zetu walikuja hapa, wakakuta kwamba wangali walikuwa wakiabudu ju—jua. Kwa sababu, katika jambo hili, waliabudu.

97 Hivyo ndivyo walivyokuwa wakiabudu miungu wa kiume na wa kike huko Rumi, wakati Mkristo alipofika Rumi.

98 Sasa, katika safari zangu, nimeona ya kwamba uabudu sanamu haujabadilika. Na wala Ukristo wa kweli haujabadilika. Zote mbili zinashikilia mahali pao, na zitafanya hivyo mpaka kule Kuja kwa Bwana Yesu. Juu ya jambo hili ningetaka kuzungumza kidogo tu, kusudi mpate wazo lake, na kama ninyi ni wa kiroho hakika mtalipata.

99 Kwa kuwa Baali alikuwa ndiye mungu-jua, vema, keki zilizotengenezwa...Naye Yeremia alisema hapa, tulilizungumzia muda mfupi uliopita, hao wanawake walikuwa wamemtengenezea keki Baali, mungu-jua. Maana, mtaona baadaye kidogo, kwamba hapo chini kwenye mlango huo, kama mkipasoma, kwamba walisema, "Tusipomwabudu Baali basi mimea yetu inaharibika, kwa maana Baali alikuwa ni mungu wa ustawishaji." Kwa maneno mengine, "Tunajua ya kwamba jua huifanya mimea kukua."

100 Lakini nabii aliwaambia, "Ni kwa sababu mmemwacha Mungu, hiyo ndiyo sababu mimea yenu haikui."

101 Lakini walimwabudu Baali, wakasema "Watamwabudu, wamtolee sadaka."

102 Sasa, kama Baali ni mungu duara. . .(Sasa, lishikeni hili, neno kwa neno, nanyi mtayapata hayo mengine, mwishoni mwa Ujumbe huu.). . .mungu alikuwa ni mungu mduara, mungu-jua, walikuwa na visahani vikubwa mno vya shaba ambavyo vingeliakisi jua na kuonekana kama moto. Halafu mkate ambao Yeremia alisema hapa ya kwamba walininii. . . wanawake wangemwokea Baali keki hizi, kwamba ilifanyizwa ya duara kama jua. Vema, basi, iliwekwa madhabahuni, madhabahu ya kipagani, kwa ajili ya ushirika, ikafanyizwa ya duara kama jua ama kama mwezi, kwa maana ilikuwa ni mungu-jua ama mungu-mwezi.

103 Yule. . .Baalimu alikuwa, ambaye tulisema, "Ndiye mungu wa ustawishaji wote, ambaye hufanya kila kitu kukua."

104 Sasa, kanisa la mwanzoni lilikuja kukabiliana na jambo hili wakati lilipoingia Rumi. Na inasemwa na kuaminiwa na kanisa la Kirumi, ama na kanisa siku hizi, ama kanisa Katoliki la Kirumi, ambalo linaitwa "Katoliki. . . "

105 Sisi sote ni *katoliki*. Sisi ndio Kanisa katoliki, sisi ni katoliki ya kimitume. Hilo *katoliki* linamaanisha "la ulimwenguni kote." Nasi ndio Kanisa la ulimwenguni kote la Imani ya kimitume. Naam, bwana. Kuna tofauti kati ya makanisa hayo mawili; moja lilikuwa ni katoliki, la ulimwenguni kote, *la kimitume*; hilo lingine lilikuwa ni Katoliki ya *Kirumi*.

106 Na ilisemekana ya kwamba Petro. . .ama wanaamini, ya kwamba Petro ndiye aliyeanzisha kanisa la Kirumi. Ninataka Maandiko, ninataka mahali unapoweza kusema ya kwamba Petro alipata kuwa Rumi chini ya hali zozote. Kama vile kanisa la Kirumi lilivyosema, "Alikuwa huko kutoka 41 hadi 46."

107 Na, kwenye wakati uo huo, Klaudia alikuwa mfalme mkuu huko Rumi, ambaye aliwafukuza Wayahudi wote. Someni Matendo, mlango wa 18, nanyi mtaona ya kwamba Paulo, wakati alipopanda kwenda Efeso, aliwakuta Akila na Prisila, ambao kweli walikuwa ni Wayahudi, nao walikuwa wamefukuzwa kwenye wakati wa hayo mateso, nao walikuwa hapa Palestina tena kwa sababu Klaudia alikuwa amewaamrisha Wayahudi wote waondoke, Wakristo na waorthodoksi pia. Akila na Prisila ndio walioanzisha kanisa huko Rumi, nao walilazimika kuondoka kwa sababu ya kuinuka kwa Klaudia, alikuwa amelifukuza kanisa lote. . .ama Wakristo na Wayahudi wote kutoka Rumi.

108 Sasa, "Petro akiwa ni askofu wa kanisa," nami ninaweza kuwaonyesha Maandiko, moja kwa moja mpaka angalau karibu miaka sabini, ya kwamba Petro kamwe hakuondoka Palestina. Moja kwa moja katika Maandiko! Nanyi mnasema ya kwamba "Petro aliuawa kinyama huko Rumi, na Paulo alikatwa kichwa chake Rumi." Hilo ni fundisho la sharti. Nimesoma vitabu vyote vya wafia imani ninavyoweza kupata, wala hakuna hata

kimoja chavyo kinachosema lolote kuhusu Petro wala Paulo (mmoja wao) akiuawa huko Rumi. Katika vile vya kweli vya wafia imani vya mwanzoni kabisa tunavyoweza kusoma, hakuna kimoja chake kinachosema lolote kuhusu hilo. Hakuwa huko! Ni fundisho la sharti.

109 Nipo hapa kuanika upagani, kwa hiyo tuta—tutafanya hivyo kwa msaada wa Bwana na Neno Lake, mnaona, kuwaonyesha tu jinsi kanisa lilivyo. Mnapiga makelele juu ya "Katoliki!" lakini ngojeni tu dakika chache.

110 Sasa, sasa, tunaona ya kwamba Akila na Prisila (kulingana na Maandiko) wakiishatolewa Urumi, maskini kanisa hilo dogo liliachwa kama yatima, wote waliokuwa mle ndani walikuwa ni wapagani walioongoka waliokuja wakaingia katika kanisa la Kikristo la Kirumi, lile kanisa la mwanzoni ambalo Akila na Prisila na mume na mke mwingine ambao walikuwa wameanzisha kanisa hili na kulilea.

111 Ndipo tunaona, mara walipoondoka, kwamba waliwafanyiza maaskofu wao wenyewe na kuchukua fundisho lao wenyewe, kisha wakachukua . . . wapate kibali cha mfalme mkuu, Konstantino na hao waliokuja baadaye, wapate kibali, kwa sababu iliwabidi kuchukua wafuasi mle ndani wapate kupigania viti vya siasa nchini. Waliwaingiza wafuasi wa kanisa, na kuwaingiza kwenye ("kamilifu") kukiri tu, huku hawajui zaidi juu ya Mungu kuliko baadhi ya watu hawa tulio nao Marekani siku hizi; ni kama tu kukiri, ambalo lilikuwa vigumu sana kwao kumkiri Kristo, Mungu mwingine mbali na mungu wao wenyewe. Na mle ndani wakaingiza, katika katiba yao ya kanisa, sherehe za kipagani.

112 Sasa, kuhani wa Kirumi, kisha wakaingiza hili kwa kula na kufanya ushirika. Jambo la kwanza lililojitokeza lilikuwa ni kufanya ushirika. Badala ya kipande kilichovunjwa kama Mwili wa Kristo, wangekitengeneza kikiwa *duara* kama jua ama kama mwezi. Na hata wa leo kingali ni cha duara! Hakika. Kingali ni mkate mwembamba wa duara, na si kipande kilichovunjwa cha Mwili Wake. Ni mviringo na laini. Makasisi wa Kirumi siku hizi huuweka mkate huu mwembamba madhabahuhi na kuuita "Mwili halisi wa Kristo."

113 Sasa, kuna ubishi mkali sana kati ya baadhi ya hawa Waepiskopolia wenye vyeo, na kadhalika. Na kanisa Katoliki uko juu ya suala hilo, kama ni Mwili *halisi* ama *unauwakilisha* ule Mwili. Wakatoliki wa Kirumi wanasema "ni Mwili halisi," kwa maana huo ulikuwa ni mwili halisi wa Baali (mungu-jua) aliyejiakisi kwenye kipande kile cha shaba nao wakaufanya duara. Hakuna meza ya Kikristo iliyo na mkate mduara juu yake!

114 Kisha walitaka kuangalia mashariki, na kadhalika, kama walivyofanya katika ibada za kipagani; na kuwaingiza

wanawake, na kadhalika, kama tu walivyofanya daima, kama vile wapagani kwa hao miungu, na kadhalika. Sasa walimshusha tu Astarte na kumwinua Mariamu, wakamfanya malkia wa mbinguni. Walimshusha Jupita na kumwinua Petro. Nao iliwabidi kupata fundisho la sharti, kusudi wafanye jambo hilo iliwabidi kuninii . . .

115 Wakati Akila na Prisila waliporudi, baada ya miaka kumi na mitatu ya utawala wa Klaudia, basi waliporudi walikuta kanisa lao limejitolea kabisa kwa ibada za sanamu, bali lilikuwa limepanuka likawa kubwa mno, kitu kikubwa.

116 Kusudi wakiingize kitu hiki, hawana budi kuiondolea Biblia mbali kabisa. Sasa, mimi ni Muairishi, nina kile wanachokiita *Kanuni Za Imani Yetu* ambacho ni cha kasisi pekee, na kadhalika. Nami ninajua jambo hili, kwa mahojiano na makasisi, kasisi hatabishana nawe kuhusu Biblia, Biblia ni kitabu kingine tu kwake. Wakati huyu hapa Askofu Sheen aliposema, hapa yapata miaka miwili iliyopita, ya kwamba "Mtu yeyote aliyejaribu kuiamini Biblia, alikuwa ni kama anayepitia kwenye maji ya matope." Hawaiamini Hiyo! Wao walianzia hapo na kusema, "Mungu yumo katika kanisa Lake, sio Neno Lake."

117 Kasisi huyu hapa juu barabarani, aliyekuja kwa ajili ya mahojiano hivi majuzi, hapa juu kwenye Moyo Mtakatifu, yeye aliniambia . . . ama kanisa hili hapa juu barabarani, ninasahau linaitwaje. Nafikiri linaitwa Moyo Mtakatifu. Yeye alinijia kuhusu ubatizo, Mary Elizabeth Frazier aliyekuwa amerudi nyuma na kuwa Mkatoliki. Alisema, "Je! ulimbatiza?"

Nikasema, "Naam."

Kasema, "Ulimbatizaje?"

Nikasema, "Katika ubatizo wa Kikristo."

Akasema, "Unamaanisha kwa njia gani?"

Nikasema, "Kuna ubatizo mmoja tu wa Kikristo."

Akasema, "Una maana gani, kwa kuzamisha?"

Nikasema, "Naam, bwana."

118 Akasema, "Basi ulimzamisha kwa jina la 'Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu'?"

119 Nikasema, "Huo sio ubatizo wa Kikristo." Nikasema, "Ubatizo wa Kikristo ni kuzamisha katika Jina la Bwana Yesu Kristo."

120 Akaliandika. Akasema, "Je! utakula kiapo hiki, pia, ama azimio hili kwa askofu?"

121 Nikasema, "Kama hawezi kuliamini neno langu, acha akae bila hilo." Nikasema, "Siapi kwa chochote." Unaona? Naye akasema . . . Nami nikasema, "Sio kuwa na kiburi, bwana, bali ninajua Biblia ilisema, 'Usiape kwa mbingu wala dunia, kwa

kuwa ndipo pa kuwekea miguu Yake,' na kadhalika. Haitupasi kufanya hivyo."

122 Akasema, "Ajabu hii, kanisa Katoliki lilikuwa likibatiza namna hiyo."

Nikasema, "Lini? Lini?" Mnaona? Bali wanasema kwamba walifanya hivyo.

123 Kwa sababu, kusema kweli, walikuwa hivyo, nasi sote tulikuwa mmoja hapo mwanzo, na linaninii . . . la asili—la asili lilitoka Pentekoste. Hapo ndipo mwanzo wa kanisa la kwanza mahali popote, mtu yeyote anapoweza kuzugumzia. Kanisa la Kikristo lilianzia Pentekoste, kwa tukio la kipentekoste, watu wa kipentekoste, ubatizo wa kipentekoste. Wote walitoka kwenye lile kanisa la mwanzoni huko Pentekoste.

124 Sasa, angalia. Sasa, tunaona ya kwamba basi iliwabidi kuondoka kwenye mafundisho ya Biblia wapate kuwa na mambo haya ya kuwapendeza wafalme wakuu na kadhalika, kuwaingiza wapagani.

125 Sasa, angalieni. Petro alikuwa ni Myahudi. Sivyo? Ungeweza kuwazia Mtakatifu Petro akichukua wazo la kuweka sanamu kanisani, Myahudi ambaye alikatazwa hata kuiangalia sanamu? Ungeweza kumwazia akifanya jambo kama hilo? Sio Petro! Ungeweza kumwazia akisema, "Maandiko yangu yote huko nyuma mwanzoni yalikuwa ni ya uongo, nitayatupa tu chini sasa. Nitaishi kama roho katika kanisa hili la Kirumi, na nitachukua . . . "?

126 Vema, ingekuwa ni mtu aliyebadilika. Kwa hiyo, kufanya hilo, iliwabidi kuanzisha fundisho la sharti kwamba "Petro alizikwa kanisani na alikuwa amewaachia Amri zote, nao walikuwa ndio kanisa asilia la Katoliki." Hao sio! Hakuna Maandiko, hakuna historia wala chochote kile kuthibitisha hilo; hamna kitu. Hawakuwa.

127 Na kasisi huyo mpagani wa kanisa la kwanza la Kirumi ni sawa kabisa kama yule aliyepo siku hizi. Wanaamini ya kwamba mkate huo ni mwili wa Kristo, ya kwamba kwa namna fulani Kristo hushuka na kuruka ndani ya kipande hicho cha mkate kilichowekwa madhabahuni (ambacho panya watakichukua usiku). Mnaona? Wanaamini . . . Na hiyo ndiyo sababu Katoliki inaamini huna budi kwenda kanisani kuabudu, kwa sababu "Mungu ni kanisa lao." Hiyo ndiyo sababu wanasujudu na kujifanyia alama ya msalaba, karibu na kanisa, kwa sababu "Kipande hicho cha mkate ni Mungu." Si kitu ila uwakilisho wa mungu-jua Baali, hamna Maandiko kwake hata kidogo! Naam, huo mkate mwembamba uliowekwa madhabahuni.

128 Sasa, kwa hiyo, hawakuyakubali mafundisho ya Kikristo kwamba . . . Ireneo, Polikapu, na hao ndugu wa mwanzoni, Paulo. Tunaona, mwanafunzi mkongwe kuliko wote alikuwa . . . aliyeishi muda mrefu kuliko wote, alikuwa ni Yohana.

Alihamishwa kwa muda wa miaka mitatu, huko Patimo, kwa maana alikuwa na shule. Alikuwa akiliandika ama kuliandaa Neno la Mungu, kulikusanya pamoja, zile Nyaraka pamoja. Walimpata pamoja na wasomi wake wakifanya hivyo, nao wakamfukuza kwa muda wa miaka mitatu (baada ya kifo cha mfalme mkuu alirejeshwa), ndipo basi akakiandika Kitabu cha Ufunuo.

129 Na ati mwanena kuhusu "Mungu katika kanisa Lake ama Mungu katika Neno Lake?" Biblia ilisema ya kwamba Neno ni Mungu.

> *Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.*
>
> *Naye Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu,* . . .

130 Mbali na hayo, fundisho lolote la kanisa lolote, acha liwe Baptisti, Presbiteri, Methodisti, Pentekoste, ama lolote liwezalo kuwa, ambalo halidumu neno kwa neno pamoja na Biblia hii, ni baya! Kwa kuwa Yohana alisema katika Kisiwa cha Patimo, Roho Mtakatifu, ama Kristo akinena naye, alisema hili, "Kama mtu yeyote ataondoa lolote kutoka kwa Hili au kuongeza chochote Kwake . . . " Kwa hiyo utaongezaje hizi ishara za kipagani za kuabudu sanamu, kufanyiza miungu watatu kutoka kwa Mmoja, na mambo haya mengine yote ya kikafiri ambayo kanisa la mwanzoni kamwe halikuyafundisha na liliyapinga?

131 Baraza la Nikea, kama alikuwa ni kiini kimoja ama viini vitatu, ule mjadala mkuu, hao wafia imani walikuja huko, baadhi yao wakiwa na—na . . . Jamaa mmoja, a—askofu, wahubiri wa kipentekoste, kwa ajili ya kuwawekea wagonjwa mikono, walimchoma mkono kwa chuma moto na kuivuruta mikono yake nyuma namna *hii*. Wengine, wakisimama, ambapo walichukua upanga na kuyang'oa macho yake, ilionekana kama ni kundi la wafia imani waliolitetea Neno hili! Haleluya! Waliichanganya damu yao na manabii wa kale. Neno hili, ndugu, Ni Neno la Mungu.

132 Wakati wapagani hawa walipoongoka, waliingiza hizi ishara katika Ukristo. Hawawezi kuitumia Biblia tena, kwa kuwa Biblia hulianika jambo hili. Nao watakwambia mara moja leo hii ya kwamba haiwabidi kuninii . . . hawaiamini Hiyo. Wanasema, "Ni sawa, bali kanisa ndilo Neno kuu."

133 Vema, tunaona jambo lilo hilo katika Pentekoste. Msipige makelele juu ya "Katoliki," wakati sisi tuna hatia vivyo hivyo, Methodisti, Baptisti, na kila moja la hayo.

134 Ninyi Wamethodisti, watakatifu sana, kwa nini mkamwua Joseph Smith basi? Hii ni Marekani na haki ya kuabudu. Siamini yale Joseph Smith aliyosema, bali hamkuwa na haki ya kumwua, kweli, yule Mmormoni.

135 Ninyi Wabaptisti, ni wangapi mmewaficha? Ninyi wengine?

136 Na Pentekoste, ni wenye hatia tu kama wengine wao, mnakuwa wenye kiburi na kundi la wanafiki. Na badala ya unyenyekevu na nguvu za Roho, mna Neno bila ya Roho. Nanyi mnasababisha madhara mengi zaidi kuliko mngalisababisha kama mngalikuwa kama hao wengine. Huko nyuma katika sherehe zao za kipagani pamoja na kila namna ya mawazo ya utatu, na upuuzi huu mwingine wote, hamwezi kuuthibitisha kwa Neno. Neno ni kinyume nao. Ni la kusikitisha jinsi gani, ni la kusikitisha jinsi gani!

137 Kwa hiyo wakati walipoliunda kanisa la kwanza la Rumi, ule Ukristo, iliwabidi kuiondosha Biblia; na kuzichukua sherehe hizi, kusudi wafanye hivyo, iliwabidi kuwa na namna fulani ya msingi, kwa hiyo wakasema, "Petro alikuwa ndiye papa wa kwanza wa Rumi. Na angali anabaki hivyo," wanasema. Vema, hebu na tuseme alikuwa, je! Petro angeyakanusha Maneno ya Pentekoste? Ungeweza kuwazia Myahudi akiziweka sanamu?

138 Na wakati ninaweza kuwathibitishia kwa Neno lililoandikwa kutoka kwenye Biblia, siku na miaka hasa, ya kwamba Petro kamwe hakuondoka Palestina ila wakati mmoja (na akashuka kwenda Babeli kwa njia ya Efrata), hakuwahi kuwa Rumi, kwa Maandiko, BWANA ASEMA HIVI! Lote ni wazo la kipagani.

Sasa tutalileta hilo moja kwa moja katika Uprotestanti.

139 Angalieni Pentekoste, pasipo kulichukua Neno. Dumu na hilo Neno nawe daima utakuwa sawa; liondokee hilo Neno, utaenda popote.

140 Hapa wakati fulani uliopita kwenye mkutano mkubwa na shule kubwa ya Kipentekoste, mwanamke mmoja aliruka juu, akinena kwa lugha, na kukatiza wito wa madhabahuni. Ndipo usiku huo wakati niliporudi humo, Billy alikutana nami huko, akasema, "Unajua nini? Yule mwanamke alisema alikuwa na ujumbe mwingine usiku wa leo atakaotoa."

141 Ndipo nikamwangalia mwanamke huyo (amekata nywele, nguo imembana sana ilionekana kana kwamba alimwagiliwa ndani yake, ameketi pale akitengeneza nywele zake, akivuta soksi zake ndefu), nilijua alikuwa akitaka kuruka juu. Naye akaruka juu, ndipo nikasema, "Keti chini." Akaendelea tu. Nikasema, "Unanisikia? Keti chini!" Loo, jamani.

142 Nilipotoka usiku huo, kulikuwako na jamaa hao wanne ama watano waliokutana nami huko nje pamoja naye, kasema, "Ulimhuzunisha Roho."

143 Nikasema, "Roho yeyote ninayemhuzunisha kwa Neno la Mungu anapaswa kuhuzunishwa." Nikasema, "Hivi Biblia haisemi ya kwamba roho wa nabii humtii nabii? Kama yeye anashuhudia, ambapo unabii ni—ni . . . Kunena kwa lugha ni

unabii kama kukifasiriwa." Nikasema, "Basi hebu na angojee mpaka nitakapomaliza, ndipo anaweza kuutoa."

Akasema, "Lakini wewe unafundisha Neno."

Nikasema, "Hilo ndilo ninalotetea."

144 Akasema, "Yeye alikuwa na jambo tofauti na jipya kutoka Mbinguni, kitu tofauti na Hilo." Kama huko sio kurudi kwenye Ukatoliki wa Kirumi sijui ni kitu gani!

145 Neno la kila mtu na liwe uongo na kila roho iwe uongo, na Neno la Mungu liwe ni Kweli. Neno la Mungu kwanza!

146 Shida ya siku hizi ni kwamba, wana funuo nyingi sana na mambo ya uongo. Ni kusujudia huko nje na kufungua moyo wao kwa pepo, badala ya kudumu na Neno la Mungu. Hapo ndipo ilipo shida, hiyo ndiyo shida. Watu, waaminifu, wanyofu, watu wazuri, bali huwezi kuwaambia. "Vema, tunaamini *hili*, kama Wapentekoste." "Tunaamini *hili*, kama Wabaptisti."

147 Ninaliamini Hili kwa kuwa ni Neno la Mungu! Ninampa changamoto mtu yeyote anisahihishe katika Hili. Mnaona? Hiyo ni kweli. Hili ndilo Neno! Dumuni na Hili, Hili ni kweli!

148 Kwa hiyo wakaunda kanisa la kwanza, kanisa la kwanza la Katoliki ya Kirumi. Na badala ya kumwita nanii... kumwita *askofu*, ambalo sikuzote walimwita, sasa wanamwita "Baba." Wangali wanamwita. Nao wanasema hapa, "Huna budi kukubali, ya kwamba mkate huu mwembamba *ni* Mwili wa Kristo. Na, kufikia hata, kasisi ni mungu, kwa kuwa Mungu anawajibika kuisikiliza sauti ya kasisi anayeubadilisha mkate huu mwembamba ukawa Mwili halisi wa Kristo." Na halafu watu werevu wanaacha hilo lishindiliwe kooni mwao! Loo, jamani! Loo, jinsi...

149 Lakini waabuduo wa kweli, maaskofu wa kweli, walidumu na Neno. Walikaa pale pale katika Baraza hilo la Nikea, walilitetea Neno hilo papo hapo. Naam, bwana. Walikuja kama wafia imani, chochote kile, bali walidumu na hilo Neno. Hawakutaka uabudu sanamu hata kidogo.

150 Nami ninataka mtu fulani anionyeshe ambapo Mtakatifu Patrick alipata kuwa Mkatoliki wa Kirumi. Hakuna kitu kama hicho! Yeye alilipinga kanisa hilo la Kirumi. Yeye alikuwa ni mpwa wake Mtakatifu Martin. Nilikuwa nikisoma hapa, na mwanamke aliyeandika ninii...Hazeltine, Bibi Hazeltine, *Dondoo za Baraza la Nikea*, alisema ya kwamba alienda kwenye kadi huko Oxford kuchukua ka—kadi ya, kuchukua ya, *Maisha ya Mtakatifu Martin*, naye jamaa huyu akasema, "Lakini hakufanywa mtakatifu na kanisa la Kirumi." Hakika hakufanywa mtakatifu, alikipinga kitu hicho! Na vivyo hivyo Mtakatifu Patrick. Watu waliodumu na Neno la Mungu walijenga shule zao wenyewe, wakayaondokea mambo ya aina hiyo.

151 Sasa, tunaona, ndivyo ilivyo siku hizi. Kanisa la Kirumi linaendelea moja kwa moja na ile ile biskuti yao duara, wakiamini ya kwamba Kristo hushuka chini na kuingia ndani. Na, sikilizeni, je! mnajua kasisi ndiye anayekunywa divai? (Wakati, wanapaswa kuinywa wao kwa wao, "Alipitisha kikombe mmoja kwa mwingine.") Lakini, katika muundo wa kipagani, makuhani ndio wanaokunywa divai. Mnaona? Mngali . . . Yote ni upagani! Hakika kabisa. Hawajali.

152 Wanakwambia, "Sitazungumza nawe juu ya Biblia yoyote." Huyo mhudumu, ama kasisi, aliniambia huko juu, kasema, "Bw. Branham, unajaribu kuzungumza juu ya Biblia, mimi ninazungumza juu ya kanisa."

Nikasema, "Mungu ni Neno!" Kweli. Sasa, vema.

153 Tunaona katika jambo hili, hata wa leo, hiyo ndiyo sababu kanisa Katoliki la Kirumi halina budi kwenda kanisani kuabudu. Wanafundishwa ya kwamba "Mungu yumo ndani ya mkate huu mwembamba wa duara, hiyo Hostia maskanini." Mnaona? Hivi hamwezi kuona huo ni upagani? Hakika, ni upagani.

154 Hivi hamwezi kuona ya kwamba watu watakaochukua chochote—chochote kinyume cha Neno hili ni wa namna ile ile? Hivi Biblia, katika Ufunuo 17, haikuliita kanisa Katoliki "kahaba"? Hivi haikuwaita Waprotestanti mama wa . . . ya kwamba yeye alikuwa ni "mama wa makahaba"? Kitu kile kile! Yeye alitoa mafundisho kutoka kwenye kikombe chake cha uchafu wa chukizo la uzinzi wake, uchafu na kinyaa, unaotengenezwa na mwanadamu tu, badala ya Neno la Mungu aliye hai ambalo ni la kweli na lisiloghoshiwa.

"Ee Mungu, uturehemu," ndilo ombi langu.

155 Ireneo alisema, niliandika muhtasari hapa yale aliyosema, kasema, "Neno la Mungu ni kama lundo zuri la lulu nzuri kubwa lililowekwa huko nje kufanyiza sanamu ya Mfalme mkuu, mwenye nguvu. Lakini," kasema, "kanuni za imani, mafundisho ya sharti, madhehebu, huzichukua lulu hizo za kupendeza na kutengeneza mfano wa mbwa nazo, na kuwadanganya wasiolifahamu Neno. Hili wanalifanya wapate kuzipotosha njia za Mungu na kuleta aibu Kwake." Haleluya!

156 Unapojaribu kulifanya Neno la Mungu kusema kitu kupatana na dhehebu lako, unachukua lulu kutoka kwenye Mwili wa Mfalme mkuu na kufanyiza sanamu ya mbwa, ama mbwa mwitu, ama nguruwe mwitu, ama chochote kile, kutoka kwake. Nawe unawadanganya wasiolifahamu Neno.

157 Haleluya! Kuna wengine walio na Roho wa Mungu, wanaolitetea Neno lililofanyika mwili. (Mungu, ongeza jeshi letu.) Neno, si kitu ila Neno! Lichukue hilo Neno ambapo Yesu alisema mle ndani, "Mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita."

158 Mahali liliposema, “Mkabatize katika Jina la Bwana Yesu Kristo”; wanalifanya “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,” miungu mitatu kutoka Kwake. Wanachukua kila namna ya mafundisho ya sharti, na kufanya mambo ya kila namna, na kunyunyizia badala ya kuzamisha. Kila kitu! Wanafanya namna fulani ya matope ya kujitengenezea kutoka kwake, badala ya kuyatia katika Lulu, katika yule Mfalme mkuu, Kristo.

Loo, Haleluya! Huyo ni Mungu aliyefanyika mwili, Kristo!

159 Wanazipotosha njia za Mungu. Wanawaacha watu waje kanisani, wanawake waliozikata nywele zao, waliojipodoa, mavazi yanayoonekana ni ya kashfa. Wanaume ni dondoadume sana, wanamwacha mwanamke awaongoze kwa sikio. Wanakuja kanisani, na wanacheza banko na bingo, na kila namna ya mambo mapotovu. Nao wahubiri na kadhalika wakiwa huko ufukoni, pamoja na wanawake uchi waliovaa nguo za kuogelea na wanaenda kuogelea, wakivuta sigara, na kujiita “watumishi wa Mungu”; wakati hekalu hili ni hekalu takatifu lililowekwa wakfu kwa Mungu, sio kwa uchafu wa ulimwengu. Ni kweli. Bali walizichukua lulu za Mungu na kufanya nguruwe mwitu kwake, ama mbwa mwitu, ama mbwa, ama kicheche, ama kitu kingine, na kuwalisha hayo wasio na elimu, wasio na maarifa.

160 Asante, Dak. Nilikuwa na moja hapa ila tu sikuwazia kuitumia, leso.

Naam, hivyo ndivyo wanavyofanya. Ireneo alisema kwe—kweli kabisa.

161 Mungu anawazia nini kuhusu haya yote? Ni kama tu yale waliyojaribu kusema, “Loo, haijalishi Kwake”? Inajalisha Kwake! Inajalisha.

162 Kwa nini akamwambia Yeremia mambo aliyomwambia basi? Ni kwa nini akasema hivyo? Inajalisha. Mungu ana njia.

163 Vipi kama Musa alisema, “Nitatoa kofia yangu badala ya viatu vyangu”? Asingaliliona lile ono. Inakupasa kuja kwa njia ya Mungu. Mungu anayo njia.

164 Kuna mengi sana tungaliweza kusema. Hebu na tugeukie tu Andiko moja hapa. Ninalo, nimeyaandika mengi. Hebu tufungue Hesabu 25, kwa dakika moja tu. Hesabu 25, tuone kama ina—inajalisha chochote kwa Mungu, au la. Hebu tuone kama inajalisha, kama kanuni hizi za imani, mafundisho ya sharti (na kadhalika) yanajalisha. “Yeye ni Mungu mwema, Yeye huachilia tu jambo hilo lote.” Haachilii! Yeye huweka kamba na kuning’iniza timazi, nawe huna budi kuja Kwake.

*Basi Israeli akakaa Shitimu, kisha watu wakaanza kuzini pamoja na wanawake wa Moabu;*

(Sikilizeni!)

*Kwa kuwa waliwaalika hao watu waende sadakani,* sadaka *walizowachinjia miungu yao; watu wakala chakula, wakaisujudu hiyo miungu yao.*

*Ikawa Israeli kujiungamanisha na Baal-peori; hasira za* Bwana *zikawaka juu ya Israeli.* (Si ajabu alisema "Usiwaombee watu wa aina hiyo"! A-ha?)

*Kisha* Bwana *akamwambia Musa, Watwae wakuu wote wa hao watu, ukamtungikie* Bwana *watu hao mbele ya jua, ili kwamba hizo hasira kali za* Bwana *ziwaondokee Israeli.*

*Basi Musa akawaambia waamuzi wa Israeli, Waueni kila mtu* mtu *wake . . . waliojiunganisha na Baal-peori.*

165 "Ua kila mmoja wao!" Mungu anataka kuwa ni Mungu, na kama Yeye si Mungu hataichukua nafasi ya pili. Haimbidi kumwacha Baali (na mafundisho fulani ya sharti ya kujibunia, na nadharia fulani ya mtu fulani, ama wazo fulani la kanuni za imani, ama wazo fulani la—la dhehebu) kumzuia, Yeye ni Mungu na anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Haimbidi kuwa na madhehebu yenu. Haimbidi kuwa na mashirika yenu makubwa na shule zenu na kadhalika. Yeye huchukua kile anachoweza kupata mkononi Mwake, ambacho ni duni, anakipulizia pumzi ya Uhai nacho kinakuwa kitu ambacho kitamtumikia. Hilo ndilo linalomfanya kuwa ni Mungu. Hakika, inajalisha kwa Mungu.

Unasema, "Haijalishi." Inajalisha! Hakika, inajalisha.

166 Papa Leo Mkuu, alitawala kutoka 440 hadi 461. Loo, aliwazia alikuwa akifanya hasa kilichokuwa sahihi, akaja kanisani . . . Kabla yake alikuwa Victor, naye alikuwa ni msaliti, pia. Naye akaja mle ndani, na jinsi alivyowaua Wakristo na kila kitu kingine.

167 Na halafu ni nani aliyeanzisha haya yote, kuifanya mauaji "yaliyohalalishwa"? Mnajua alikuwa ni nani? Mtakatifu Agostino wa Hippo, huyo ndiye hasa aliyefanya hilo.

168 Mtakatifu Agostino alikuwa na nafasi wakati mmoja, ndivyo inavyosema historia, ya kuwa mtu mashuhuri na kujazwa na Roho Mtakatifu. Aliketi nyuma ya ua kule, huko Lyons, Ufaransa, kwenye ile shule kuu ambamo Ireneo alikuwa amefundisha, na hao pamoja na Mtakatifu Martin. Yeye aliketi kwenye ua wa shule hii na Roho Mtakatifu akamjia, bali alikataa kumpokea.

169 Basi alifanyika nini? Mwana wa kuzimu maradufu kuliko alivyokuwa hapo mwanzo, akashuka akaenda moja kwa moja mpaka Hippo, Afrika, hapo akaanzisha shule yake. Nayo ilikuwa . . .

"Nionyeshe!"

170 Ninaweza kukupeleka kwenye historia. Yeye ndiye aliyetoa idhini yake kwake, kwamba “Ilikuwa ni sawa kumwua mwasi yeyote ambaye angeyakanusha mafundisho ya sharti ya kanisa la Kirumi,” Mtakatifu Agostino wa Hippo. Je! kuna mwanachuoni wa Biblia hapa, ama mtu fulani ambaye amesoma historia, anayejua kuwa hiyo ni kweli, inua mkono wako? Naam, mnaona? Hakika wako. Mtakatifu Agostino wa Hippo, yeye ndiye aliyepitisha uamuzi kwamba “Ilikuwa ni halali kuwaua waasi waliolipinga kanisa la Kirumi.” Kuidhinisha hayo mafundisho ya kipagani, ya kuiacha Biblia, na kuanzisha ibada ya kuabudu mungu-mwana. Mnajua sababu ya Ukristo kuninii . . .

171 Mnajua mahali mlipoipata Krismasi? Kristo alizaliwa Aprili, lakini wao walifanya nini? Mfumo wa jua unapunguza mwendo sasa wakati ukiondoka, kila siku ikiendelea kuwa ndefu zaidi, ama fupi kidogo, na fupi kidogo, na kutoka tarehe ishirini mpaka ishirini na tano ndipo mungu-jua alipokuwa na siku ya kuzaliwa kwake. Yapata tu siku tano pale, hapo ndipo walipokuwa na sarakasi za Kirumi kwenye wakati huo, sherehe za siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua wakati huo. Basi sasa mnaona kile mlicho nacho sasa? “Walisema ifanye kuwa ‘mungu jua,’ acheni tuichukue ‘Mwana wa Mungu.’” Na kitu hicho chote kwanza kabisa ni upagani! Nao watu mitaani pamoja na viatu vyao vyenye visigino virefu, na wanajinyonganyonga huku na huko mitaani, wakikimbia madukani.

172 Na hapa hivi majuzi mke wangu alikuwa akiniambia, “Mtu fulani alisema, ‘Sijui kile nitakachomnunulia Baba.’ Kasema, “Ndugu yangu atamnunulia kwati la wiski, na huyo mwingine akasema atamnunulia shampeni.’ Na mmoja akasema, ‘Vema, nitamnunulia se—seti ya karata.’” Sherehe za Krismasi, upagani, ibada za ibilisi! Vema.

173 Lakini Agostino aliziidhinisha. Kama ukitaka kurejea kwenye haya katika kile cha Schmucker, kitabu cha Schmucker, S-c-h-m-u-c-k-e-r, *Matengenezo Matukufu* kilichoandikwa na Schmucker, hiki hapa kilichosema, ya kwamba “Tangu wakati Mtakatifu Agostino wa Hippo alipopitisha uamuzi huu kwa kanisa Katoliki, ilifungua milango wazi kabisa kwao kuua chochote walichotaka kuua wakati huo, kilicholiasi hilo kanisa la kipagani. Na kuanzia wakati wa Mtakatifu Agostino, karibu miaka mia tatu baada ya Kristo, mpaka 1850, yale mauaji makuu ya Ayalandi, kulikuwako na Waprotestanti milioni themanini na sita waliouawa na kanisa Katoliki. Hiyo iko kwenye orodha ya ufia imani wa Kirumi, ‘Milioni themanini na sita.’” Sasa gombana na mwanahistoria huyo, yeye ndiye aliyesema jambo hilo. Mimi ninarudia tu neno lake. “Kila mmoja asiyekubaliana na fundisho la sharti la Katoliki!”

174 Sio *katoliki*, neno katoliki, hawaninii hawalistahili jina hilo. Hao ni wapagani wa Kirumi.

175 Sio hao watu wa thamani. Kuna makumi elfu ya hao watu huko nje, waaminifu tu kama hao . . . mwabudu sanamu mwingine yeyote alivyo. Wanadhani kwamba wanamwabudu Mungu, wakati (rudini kwenye Neno) wako katika sanamu huku sanamu zikiwa zimetapakaa mahali hapo pote. Mnaona!

176 Vema, ilikuwa ni fundi- . . . fundisho la sharti, mafundisho ya sharti ya Kirumi. Na, sikilizeni, ninataka kutaja jambo fulani hapa. Nililiruka hilo.

177 Katika mwaka wa 1640, katika mwaka wa 1640, wakati mauaji ya Ayalandi yalipotokea, chini ya majesuiti wa Kirumi na makasisi, waongofu elfu mia moja wa Mtakatifu Patrick waliuawa. Kama Mtakatifu Patrick alikuwa ni Mkatoliki wa Kirumi, basi kwa nini wakawaua watu wao wenyewe? Hao walikuwa ni wafanya kazi wa viwandani, na wowote wale. Hiyo ni kweli. "Elfu mia moja," kwenye ufia imani, "ambao waliwaua kwa kuwa walitofautiana na mafundisho hayo."

178 Nimekuwa kwenye baadhi ya makanisa ya Mtakatifu Patrick huko Ayalandi ya Kaskazini. Naam, bwana. Nilikuwa na majaliwa ya kuona jambo hilo. Lilikuwa tu ni jengo kubwa la kale. Hawakuwa na sanamu hizo zilizotokeza, na kumwaga vitu miguuni mwao, na kuwalipia hao watu kurudi na kuingia katika sanamu hiyo. "Maria, salamu, Maria, na mama wa Mungu," jambo lile lile walilofanya kwa Astarte (kufanyia uchawi), roho ya Mariamu.

179 Miaka miwili tu ama mitatu iliyopita kanisa Katoliki lilianzisha fundisho jipya la sharti kwamba "Mariamu alikuwa amefufuka katika wafu na ameenda Mbinguni." Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Loo, ninyi nyote mnakumbuka, hakika, magazeti yalijaa hayo. Mafundisho ya sharti! Limejengwa juu ya mafundisho ya sharti, na hamna chembe ya Kweli mahali popote.

180 Sasa, ninyi Waprotestanti ni wabaya tu vivyo hivyo, ambao mnakataa kulichukua Neno la Mungu. Ni fundisho la sharti la kanisa la Kiprotestanti sawa na lilivyo fundisho la sharti la kanisa Katoliki, nasi sote kwa jumla tumekosea mpaka tutakapolirudia Neno la Mungu aliye hai! Kweli.

181 Ninyi Assemblies of God, ninyi Foursquare, ninyi Wapentekoste wa umoja, utatu, ama chochote mlicho, rudini kwenye Neno la Mungu! Achaneni na baadhi ya hizi sanamu za kimadhehebu, sfiniksi za kimadhehebu. Wanajiroga wenyewe (roho wa ibilisi) wanajiingiza kwenye sanamu hizi za kimadhehebu. Mnajua hilo? *Dhehebu* ni "sanamu"!

Unasema, "Je! wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mpresbiteri."

"Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti."

"Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mpentekoste."

182 Hilo halimaanishi zaidi ya vile kusema wewe ni "nguruwe mwitu" ama "mbwa" ama "kicheche," halina uhusiano Nalo. Hiyo ni kweli. Tunachohitaji leo hii ni: kurudi kwenye Neno la Mungu!

183 Sasa, kuhusu hawa wafanyakazi madukani na watu wa thamani wa Ayalandi ya Kaskazini, ikiwa Mtakatifu Patrick . . . ambako shule zake zote zilikuwa. Mwajua, jina lake halikuwa Patrick? Jina lake lilikuwa Succat. Alitekwa nyara akiwa mvulana mdogo; dada zake wakauawa. Naye akarudi, kwa kuwa aliwafundisha mbwa kuwakimbiza nguruwe mwitu na kadhalika, kwa hiyo a—a—a—akafanya hivyo, wakati alipofanya hivyo, ndipo wao . . . akapata njia ya kurudi nyumbani kwa baba na mama yake. Ndipo akaanzisha shule. Nayo shule hiyo huko Ayalandi ya Kaskazini kamwe haikumkubali papa kama halifa mkuu wa Mungu, hawakuamini hilo. Walidumu na Neno. Mungu na ambariki mtakatifu huyo aliyebarikiwa, Mtakatifu Patrick, mtu mashuhuri.

184 Na unawasikia wakisema ya kwamba "Mtakatifu Patrick aliwafukuza nyoka wote kutoka Ayalandi." Isome historia na uone ilikuwa ni kitu gani. Mtakatifu Patrick aliamini katika kunena kwa lugha. Mtakatifu Patrick aliamini katika kuwashika nyoka ama kunywa vitu vya kufisha; na wakati angemshika nyoka na kumtupilia mbali naye, wao walisema, "Aliwafukuza nyoka kutoka Ayalandi." Ilikuwa ni kwa sababu yeye aliamini katika kuwashika nyoka, na hakuna kitu kingewadhuru. Naam, loo, hakika.

185 Hawakuwa na hayo . . . haya madhabahu makubwa mno. Na mtakatifu ange—angefanya nini . . . Ireneo angefanya nini leo hii? Mtakatifu Patrick angefanya nini leo hii, kuona mamia ya mabilioni ya dola yamewekwa katika Ukatoliki wa Kirumi, kujenga makanisa makubwa na sanamu za mamilioni ya dola na kila kitu kama tu vile Waprotestanti wanavyofanya?

186 Nilitoa tamshi hivi majuzi nalo likakwaza kila mtu, hiyo ndiyo sababu ninaishikilia kanda hii. Achaneni tu nao, kipofu akimwongoza kipofu mwenziwe, waacheni waanguke shimoni. Hilo ndilo jambo pekee unaloweza kufanya, unaona. Nilipowaambia juu ya miito ya madhabahuni, hakukuwako na kitu kama "miito ya madhabahuni" katika Biblia.

187 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . juu ya utakatifu Wake. Kwa kujinyenyekeza wenyewe kwa kifo Chake, tukijihesabu kuwa si kitu, ndipo Roho Mtakatifu anaingia na kutuinua juu. Ndipo hatujitegemei, maana hatuwezi kufanya lolote, bali tukiwa na Yeye tunaweza kufanya mambo yote.

188 Sisi, katika sura Yake, sura hai ya Mungu aliye hai. Ni kitu gani una . . . Unapojisalimisha mwenyewe kwa Mungu na

Mungu anaingia ndani yako, inakufanya nini? Sura iliyo hai ya Mungu. Si sanamu iliyokufa iliyowekwa pembeni; si dhehebu huko kwenye makao makuu Washington, katika—katika—katika Muungano wa Makanisa; la, hiyo ni sanamu iliyokufa, sanamu iliyokufa na kanuni ya imani iliyokufa. Lakini sura iliyo hai katika mtu binafsi!

189 Mtu fulani alikuwa akifundisha hivi majuzi, ama alikuwa na muhtasari mdogo, na mtu fulani akasema ya kwamba "Kama mtu hakuwa ameokolewa, na . . . Kama mwanamume alikuwa ameokoka na mke wake hakuwa ameokoka, wangeenda katika Unyakuo? Mwanamke huyo asingeenda katika Unyakuo, kusingekuwako na kitu kama mwanamke kwenda katika Unyakuo ati kwa sababu wao ni mmoja." Upuuzi! Yesu alisema, "Watakuwako wawili kitandani, na nitamchukua mmoja na nimwache mmoja." Ni jambo la kibinafsi kati yako na Mungu, kuutoa mwili *wako*; kama mama, baba, watoto, chochote kile analipokea au la. Amina!

190 Ee Mungu! Ulimwengu huu mwovu, mchafu, wenye kinyaa; makanisa haya machafu, yenye kinyaa yanayojiita makanisa; madhehebu haya machafu, yenye kinyaa; hizi kanuni chafu za imani, zenye kinyaa ambazo zinalipinga Neno la Mungu. Ee Mungu, mlete maskini mtu mnyenyekevu mahali fulani na kuyasafisha kabisa, na kuyainua katika ulimwengu wa Roho na ujionyeshe Mwenyewe, Mwenyezi Mungu. Amina. Limekuwa ni kitu kiovu jinsi gani!

191 Tunafanywa washiriki wa utakatifu Wake. Sisi, katika sura Yake, ni sura zilizo hai za Mungu aliye hai. Halafu, tumekufa kwa nafsi zetu wenyewe, tukafufuka pamoja Naye, (sasa sikilizeni, sikilizeni hili), Neno Lake likafanyika mwili tena ndani *yetu*. (Loo, Ndugu Neville!) Angalia! Ni kitu gani? Sio mungu wa kisasili, wa kuwaziwa anayeketi pale nje, bali ni Mungu aliye hai. Mungu aliye hai ni nini? Neno ndani yako likijifanya halisi. Whiu! Utukufu kwa Mungu! Loo, najua mnafikiri mimi ni mtakatifu anayejifingirisha, labda ndivyo nilivyo. Lakini, loo, ndugu, mnaliona? Ameshinda kila dhehebu, ameshinda upagani wote, Mungu aliye hai aliyedhihirishwa katika hekalu lililo hai, na Neno la Mungu (ambalo ni Mungu) limefanyika mwili ndani yako. Kwa nini? Umeketi katika ulimwengu wa Roho, umeshinda vitu vyote, katika Kristo Yesu. Amina!

Loo, ninalipenda tu. Sina budi kuruka jambo fulani na kuendelea.

192 Sasa, sikilizeni. Basi aliye mdogo kuliko wote wa waaminio Wake, haidhuru ni mrefu ji—jinsi gani, ama na—nani, mdogo, au chochote ulicho, aliye mdogo kuliko wote wa waaminio Wake (ndani Yake) ameweka uovu wote chini yao. Mnaona? Angalieni! Kristo Ndiye Kichwa cha Mwili huo. Hiyo ni kweli?

Vema, popote Kichwa kilipo mwili upo pamoja Nacho. Utukufu! Mahali kichwa changu kiendapo kinauchukua mwili wangu pamoja nacho. Na mahali alipo Yesu, Kanisa lipo pamoja Naye. Amina! Yeye hatoki kwenye Neno Lake; Yeye hudumu katika Neno Lake, analiangalia, kulidhihirisha. Kanisa Lake liko pamoja Naye.

193 Na, angalia, unasema, "Lakini, Ndugu Branham, mimi ndiye niliye mdogo kuliko wote." Huyo ni nyayo za miguu Yake. Lakini, kumbuka, Yeye ameshinda pamoja na wewe, akashinda pomoja nawe juu ya kila kitu, hata kama wewe ni nyayo za miguu Yake. Kila ugonjwa, kila pepo, kila mamlaka, hata mauti yenyewe, yako chini ya miguu yako, chini *yako*. Utukufu! Sijisikii kama nilikuwa na umri wa miaka hamsini na miwili asubuhi ya leo. Hii ni Kweli. Kama ninaweza tu kulifanya kanisa hili lione hilo, ndugu, tutakuwa kanisa lililoshinda. Waaminio ndani Yake, maovu yote chini Yake. Loo, utukufu!

194 Ninaenda kuchunguza kidogo, nitaanza tena wakati mwingine.

195 Sikilizeni, sikilizeni hili. Mnasema, "Ndugu Branham, sina nguvu." Wala mimi nami. Sina nguvu zozote. "Vema, Ndugu Branham, mimi ni mnyonge." Nami pia. Lakini sizitegemei nguvu zangu, si nguvu zangu. Ninategemea mamlaka yangu, unaona, mamlaka yangu niliyopewa. *Mimi* siye aliye na nguvu, sina nguvu. *Yeye* yuna nguvu, na mimi—mimi ni Wake.

196 Hapa, namna hii, tuseme kwa mfano, huu hapa msongamano wa magari ukishuka kuja barabarani, kwenye Barabara Kuu ya Nne huko Louisville, "Vuum, vuum, vuum, vuum," upesi tu yawezavyo, maili sitini kwa saa kuvuka barabara hiyo, kila mtu akienda kasi, yakisongamana, kusukumana. Mtu mmoja mdogo anaenda pale, anainua mkono wake, na, ndugu, breki zinafungwa. Vema, mtu huyo mdogo hana nguzu za kutosha kusimamisha moja la magari hayo, bali anayo mamlaka. (Utukufu!) Si nguvu zake. Vema, kama moja la magari hayo lingemgonga, lingemwangamiza kabisa. Lakini acha ainue mkono wake! Kwa nini? Madereva wa magari hayo wanaitambua sare hiyo.

197 Loo, ndugu, wanaitambua sare hiyo, nazo breki zinalia. Kwa nini? Angalia mamlaka yake. Angalia kilicho nyuma yake. Mfumo wote wa mji uko nyuma yake. Walinda sheria wa mji wako nyuma yake. Sare hiyo inawawakilisha hao. Yeye ni tofauti, naam, bwana, kwa kuwa ni afisa.

198 Akipaza sauti, "Simama!" Vema, moja la hayo magari liende "vuum," na kumfagilia mbali hivyo. Lakini afadhali wasithubutu hilo, waangalie kilicho nyuma yake. Watatia breki na kuteleza. Hata haimbidi kusema kitu, ni kuinua tu mkono wake. Hilo latosha, hakika. Mamlaka yake yanatokana na walinda sheria, wote wako nyuma yake. Mwenyewe, yeye ni

mnyonge, lakini ni nini kilicho nyuma yake? Hicho ndicho kinachoninii . . . vazi lake, yeye amevaa sare.

199 Hiyo ndiyo ninii . . . sio sanamu, bali kile mtu binafsi anavyopaswa kuvalia. Na tuvae silaha zote za Mungu, amina, dirii ya wokovu, ngao hii kubwa mno (ukubwa wa mlango) ya imani. Loo, ndugu. Si kile alicho yeye, bali ni kile anachowakilisha.

200 Hicho ndicho afisa huyo . . . si mtu huyo mdogo anayesimama pale, yeye ni mtu wa kawaida tu, bali ni kile anachowakilisha!

201 Silaha zetu ni Yesu Kristo. Naam, bwana. Pepo wote wanafunga breki zao wanapoiona Hiyo. Wanapoiona hiyo silaha yote ya Mungu, ubatizo wa kweli wa Roho Mtakatifu, amina, wanapoiona ikija moja kwa moja kutoka kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, umevaa silaha yote ya kufufuka Kwake. Amina.

202 Sio kwamba *wewe* una nguvu, wewe si kitu, bali ni kile kilicho nyuma yako. Kwa nini? Wewe umekufa. Ulijiunga na jeshi, umejiunga na kikosi cha polisi, utalinda sheria na kuwadhibiti pepo hawa. Hiyo ni kweli, uko kwenye kikosi cha polisi, kitu hicho chote kiko nyuma yako. Unaona, umehesabiwa umekufa, wewe si kitu, usingeweza kusimamisha chochote. Bali mamlaka yako uliyopewa, kwa kuwa umefufuliwa na umeketi katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, ibilisi anatambua hilo. Kila kitu kinafunga breki zao wakati mikono hiyo inapoinuliwa.

203 Mtakatifu Martin, wakati mmoja kotini . . . Kulikuwako na mtu mmoja kule akikwaruza (ibilisi), alikuwa akiuma vipande vikubwa kutoka kwa watu namna hiyo, nao watu walikuwa wakikimbia, alikuwa akijaribu kuwaua. Akachukua konzi kubwa . . . alikuwa na pembe kubwa mno, meno, alikuwa aking'wafua vipande vikubwa vya nyama namna hiyo wakati akifanya vurugu huko.

204 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . katika waabuduo. Na siku alizoona mbele, na akajua ingekuwa hivi, wakati Yeye mwenyewe angefukuzwa kutoka kanisani Mwake, kanisa la Laodikia. Yeye alisema, "Tazama, nasimama mlangoni na kubisha." Shirika hilo lilikuwa limemfukuza, nao wamefanya hivyo siku hizi, bali Yeye anasimama mlangoni kubisha.

205 Ee Mungu, jalia washiriki wa Mwili Wake watambue leo hii ya kwamba tuko katika Kanisa lililoshinda. Tumo—tumo katika Kristo. Tumeketi juu ya mambo haya yote ya ulimwengu.

206 Kwa nini wanawake wetu wapende kukata nywele zao? Mungu, inaonyesha kuna kasoro fulani. Mbona wangetaka kujianika wakiwa na vitu vinavyoonekana vya kuvutia kimapenzi? Ni kwa nini watu wetu wapate njaa mioyoni mwao kumsikiliza ja—jamaa kama Elvis Presley ama—ama baadhi ya hawa akina Riki, ama kadhalika, wanaosimama pale na maskini gita na mziki huo wa kung'orota na kuwafanya wasichana wetu

wadogo wayumbeyumbe na kuondoa nguo zao za ndani, na kadhalika? Mungu, na halafu mvulana huyo anadai kwamba ni Mpentekoste! Ee Mungu, ni nini. . .Mwangalie huyu Pat Boone anayedai ni wa Church of Christ na mambo haya yote ya kuchukiza, na kitu kichafu. . .Ee Mungu, akijiita anatoka "katika Church of Christ."

207 Mungu, tunatambua ya kwamba beji ya mamlaka sio jina la dhehebu fulani, bali ni nguvu—nguvu za kufufuka kwa Kristo katika maisha ya kila mtu binafsi. Mungu, jalia watu hawa hapa asubuhi ya leo wajitahidi kuingia katika Hizo. Na kama kanda hii ikiwahi kupelekwa kwenye nchi iliyokaliwa na watu, Bwana, jalia wajue ya kwamba halikusemwa kwa nia mbaya, maana mimi mwenyewe ningekuwa makosani, bali ni kwamba Kanisa lipate kushinda na kutambua mahali pake. Ili wapate kuona ambapo sanamu hizi zote. . .Mahali kanisa Katoliki lilipotokea dhahiri na kulifanya "sanamu," Waprotestanti wanalifanya "dhehebu," nao ni wabaya tu vile vile; wakilikana Neno, "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake." Ee Mungu, jinsi Neno Lako lilivyo la kweli, kila Neno!

208 Sasa tunaomba, Baba, ya kwamba utatusamehe dhambi zetu, na jalia Ujumbe huu uzame kwenye kilindi ndani ya mioyo. Na jalia watu. . .Lijalie kanisa hili, kama vile maskani hii ndogo sasa iko kwenye harakati za ujenzi wa kujenga kanisa, jalia kamwe wasitazamie kitu fulani cha kupendeza, bali pa kutosha tu kuwasetiri watu. Mungu, jalia kamwe wasiende kuangalia na kusema, "Sisi ni wafuasi wa maskani kubwa ambayo imefunikwa na kuba kubwa." Mungu, jalia liwe ni ganda tupu. Jalia kamwe wasipoteze lile Ono, la Yesu Kristo. Jalia awe Ndiye anayelijaza hekalu lao, ndipo nguvu na moto wa Roho Mtakatifu utashuka juu ya madhabahu ya mioyo yao. Hapo ndipo palipo na madhabahu halisi, Bwana, ni juu ya moyo wa kila mtu binafsi.

209 Ninaomba asubuhi ya leo ya kwamba Neno hili litakaa kwa uzito sana katika madhabahu ya kila moyo hata hawataweza kuliondokea kamwe, hata wataijia Injili kwa akili timamu na kwa busara, wakiyaamini Maneno; hata wasifungue moyo wao kwa nguvu za pepo (ama mihemko, ama vilio vyembamba, ama kuruka-ruka, ama—ama dhihirisho fulani, namna fulani ya kimwili, ama kitu kama hicho), bali kwa Roho halisi wa Kristo, wa kweli na wa upendo, ambapo atajidhihirisha Mwenyewe katika upendo na uweza.

210 Tujalie, Bwana. Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha *Nampenda*—Mh.]

. . . Nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

211 Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, ni wangapi watakaoweka moyo wenu madhabahuni na kuufanya shamba kwa Mungu, ili apate kulipanda Neno Lake juu ya madhabahu ya moyo wako, litakaloleta maisha ya ufufuo wa Kristo? Mwaweza kuinua mikono yenu na kusema, "Mungu, ninatamani hili kwa moyo wangu wote"? Mungu na aibariki mioyo yenu iliyo na njaa, madazani baada ya madazani.

Uache huko, uache tu huko,
Upeleke mzigo wako kwa Bwana na uuache huko;
Kama tukiamini wala tusitie shaka, hakika Yeye atatutoa;
Tupeleke mzigo wetu kwa Bwana na tuuache huko.

212 Moja kwa moja moyoni mwako, mkumbuke Kristo aliye Mwokozi, kumbuka alikufa kwa ajili yako. Na kama tu utajifia mwenyewe, hiyo itaufanya tupu mwili wako, ifanye tupu nafsi yako, iufanye tupu moyo wako kwa kila kitu cha ulimwengu huu na anasa zake zote, ndipo Kristo . . . utafufuka pamoja Naye.

213 Kama hujabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, kuna kidimbwi kilichojaa maji hapa. Na, utakapotoka kwenye maji hayo, unafufuka upate kutembea pamoja na Kristo katika maisha mapya. Umekufa basi, wewe hupo tena . . . hasira na kila kitu zimeondoka. Wewe ni kiumbe kipya katika Kristo. Ndipo anakufufua kwa Roho Mtakatifu na kukuweka katika ulimwengu wa Roho pamoja Naye, juu sana kuliko nguvu zote za ulimwengu huu.

214 Haidhuru ulivyo mdogo, kama wewe ni maskini mwanamke wa kuosha nguo, kama wewe—kama wewe ni ndugu tu asiye na ninii yake . . . asiyejua ABC zake, haileti tofauti yoyote kwamba wewe u nani. Wewe umo ndani ya Kristo, umeshinda mambo yote. Na mamlaka yako yako juu ya kila pepo na kila mamlaka ambayo ibilisi anayo. Wewe umo ndani ya Kristo, umeshinda.

Wakati mmeinamisha vichwa vyenu:

215 Ninajua ya kwamba kuna ndugu amekuja hapa asubuhi ya leo, Ndugu Slink (ninaamini walimwita "Sink, Jim Sink"), ambaye ninaamini kwamba ni . . . Naye ndugu yetu hapa anatambulikana kuwa ni mwalimu wa Neno hili. Hiyo si ni kweli, Ndugu Sink? Tunapaswa kumwekea mikono asubuhi ya leo kabla tu ya kuwaombea wagonjwa, kumtenga kama mhudumu (mmoja wa ndugu zetu) aende makanisani akaihubiri Injili.

216 Ndugu Jim Sink, waweza kuja hapa madhabahuni? Njoo, Ndugu Neville. Ndugu Junie Jackson, upo hapa? Mhudumu mwingine yeyote wa Imani hii?

217 Ndugu Jim Sink hapa anaiamini Injili hii tunayoihubiri, Mwana wa Mungu, kuamini ya kwamba Yeye kweli ni Mwana wa Mungu aliyezaliwa na bikira. Hiyo ni kweli, Ndugu Sink? [Ndugu Jim Sink anajibu, "Amina!"—Mh.] Je! unaamini ya kwamba Yeye alikufa na akafufuka siku ya tatu, akashinda kila kitu, na ameketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, katikati ya uweza wa Mungu huko Juu, na anaishi milele kutuombea sisi? ["Amina!"] Je! unaamini katika ubatizo wa maji katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi? ["Amina!"] Unaamini katika ubatizo wa Roho Mtakatifu kama tu vile Mungu atakavyoutoa, pamoja na ishara na maajabu kumfuata mwaminio? ["Amina!"] Yeye anaamini hayo. Nami ninaamini alikuwa na maisha yasiyo na lawama mbele za watu. Yeye anahubiri hapa kanisani, mara nyingi kwa ajili yao hapa, nami nimemwona, "mtu mzuri sana wa Mungu."

218 Sasa, kwa kanisa hili, je! kuna neno lolote humu ndani, mtu yeyote aliye na neno dhidi ya Ndugu Sink? Liseme sasa la sivyo utulie milele. Ni wangapi wanaoamini ya kwamba kwa kuhubiri Ujumbe huu na Neno hili ya kwamba Ndugu Sink . . . nawe unaamini kwamba kwa ushuhuda wa Roho Mtakatifu, ya kwamba Ndugu Sink anapaswa kuwekewa mikono na kutumwa kutoka kwenye kanisa hili hapa kama mhudumu wa Injili, kuzitangaza Jumbe hizi kama vile zimehubiriwa asubuhi ya leo, kila mahali anapoweza kwenda ulimwenguni Bwana atakapomtuma? Inueni mikono yenu na kusema, "Nitakuwa nikikuombea, Ndugu Sink." Mungu akubariki.

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

219 Ndugu Neville, kama utamwekea Ndugu Sink mikono yako wakati ukiweka mkono wako juu ya Biblia.

220 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea, asubuhi ya leo, mtu ambaye ametolewa kutoka kwenye upotovu wa ulimwengu huu, amejihesabu mwenyewe amekufa kwa nafsi yake na amemkubali Kristo kama Mwokozi, amebatizwa katika Jina la Yesu Kristo, akafufuka pamoja na ahadi ya kumpokea Roho Mtakatifu, na sasa yuko katika ulimwengu wa Roho, na anahisi wito wa huduma maishani mwake.

221 Ee Mungu, kama wazee wa kanisa hili, kama kusanyiko na waangalizi kwa jumla na kadhalika, kuliangalia kundi ambalo Roho Mtakatifu ametufanya walinzi wake, kundi hilo likiinua mikono yao ya kwamba wanamfahamu Ndugu Sink, "ya kwamba ni mtu mwenye haki," hivyo basi tunaweka mikono yetu juu yake, mimi pamoja na Ndugu Neville, kama wazee Wako, na kwa njia hii tunaomba ombi la imani na kumwekea mikono Ndugu Jim Sink aingie katika huduma ya Yesu Kristo. Tujalie.

Jalia ajazwe na nguvu za Mungu. Jalia asipatane kamwe. Jalia awalete watu Kwako.

222 Na, Mungu, tunaahidi uaminifu na udugu wetu kwake, kumuunga mkono popote alipo, katika maombi, na katika usaidizi, na vyovyote tuwezavyo. Mpokee, Ee Mungu, tunapomtoa Kwako. Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Amina. Amina.

223 Huku mikono yako ikiwa juu ya Neno, na hapo Ndugu yangu Sink, ninakuweka wakfu kama ndugu katika Kristo na ushirika wetu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina. Mungu akubariki. Vema. Nalo kusanyiko likasema, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Mungu akubariki. Kuna mengi ya kufanya katika Injili, inahitajika sana, tuko nyuma yako asilimia mia moja pamoja na kila kitu tunachoweza kufanya kusaidia. Mungu akubariki.

224 Hivi Yeye si ni wa ajabu kuwa ninii. . . Loo, jamani! Ninapenda kumwona mtu. Hilo ni sawa. Yeye ni, ninavyofahamu sasa, anachukua uchungaji wa Maskani ya Holiness huko Utica, Indiana, ambako anaishi sio mbali na hapo.

225 Sasa, hebu tuone. Loo, tunao hao ndugu? Loo, naamini tuna wagonjwa wa kuombewa bado, sivyo? Vema, je! walininii. . . ulisambaza kadi za maombi? Vema, hebu tuite kadi chache za maombi upesi sana, kila mtu na akae tu kimya kwa muda mfupi. Tumechelewa kweli. Mwaweza kunipa dakika kumi? Vema. Kadi za maombi, hebu watu walio na ninii za maombi. . . Ulizisambaza kuanzia wapi, moja?

226 Vema, kadi ya maombi namba moja, waweza kuja, namba mbili, namba tatu, namba nne, namba tano. Kadi ya maombi namba moja, mbili, tatu, nne, tano, simameni papa hapa, upesi tu mwezavyo sasa, kama unaweza kusimama. Kama huwezi, vema, hebu na tujue, tutakuja kukubeba. Tutajaribu kupata wengi tuwezavyo. Moja, mbili—mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi; sita, saba, nane, tisa, kumi; na ni wawili tu waliosimama kati ya hao. Kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. (A-ha?) Wote, kadi zote za maombi, sogeeni upande *huu* mwingine, njoni upande huu hapa, upande huu mkiweza.

227 Loo, hivi si Yeye ni wa ajabu? Sasa, kila mtu kuwa tu na kicho uwezavyo, karibu dakika kumi sasa, kama tu dakika kumi. Sasa, wale walio na kadi za maombi, tulitoa tangazo kwamba "Watu wanaotaka kuombewa, waje na kadi zao za maombi," na ili tusininii. . . Mnaona, wanaendelea kurudi, halafu wanajaribu kutumia karama za Mungu kama ubao wa kuagulia wa Ouija, bali hatu—hatuamini katika kufanya jambo hilo.

228 Tu—tunaamini katika kumwacha tu Mungu afanye Kazi Yake. Mnaamini hilo? Ni wangapi wanaoamini Ujumbe huu asubuhi ya leo kuwa ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina!"—

Mh.] Asanteni. Asanteni. Mungu awabariki. Ninauamini kwa moyo wangu wote, nafsi, na nia.

229 Sasa, inaonekana kana kwamba tuna watu kama hamsini hapa wa kuombewa, kitu kama hicho. Sasa, sikilizeni. Sasa, kila mmoja wenu yumo ndani ya Kristo. Mko katika Kristo Yesu, mmeshinda maradhi yote. Nyote mlio kwenye mstari wa maombi, ambao ni Wakristo, waaminio waliozaliwa mara ya pili, inueni mikono yenu. Mahali penu basi ni ndani ya Kristo. Tayari mmeshinda, na jambo pekee mnalopaswa kufanya sasa ni kukubali na kuamini yale Mungu amesema kwamba ni Kweli.

230 Nisingeweza kabisa kuchukua mstari huo kwa utambuzi, ingekuwa ni vigumu sana kufanya, ingetuchukua muda mrefu sana. Isingekuwa kwangu, ninaamini ningekaa hapa siku nzima, ninajisikia tu vizuri. Ninajisikia tu vizuri. Ninajua kwamba Hiyo ni kweli. Bwana asifiwe! Lakini *sasa* tumo katika Kristo, *sasa* tumeketi mahali petu katika Kristo. Amina! Loo, jamani! Je! mambo haya niliyofundisha ni Kweli? Kama ni Kweli, basi Yeye atajionyesha Mwenyewe. Hiyo ni kweli.

231 Ni wangapi wenu ninyi watu mlio kwenye mstari wa maombi hatufahamiani? Ninawajua wengi wenu, bali baadhi yenu ni wageni. Inua mkono wako, unayejua sijui lolote kuhusu shida yako, inua mkono wako; kote mstarini, a-ha, vema. Je! Yeye ni Kristo? Unaamini Hilo? Huna budi kuwa na imani, huna budi kuliamini. Kama huliamini, basi halitafanya kazi. Huna budi kupajua mahali pako, huna budi kuijua sehemu yako. Hiyo ni kweli, Ndugu West? Hiyo ni kweli. Jua mahali pako, Kristo aliahidi "Mambo nifanyayo Mimi ninyi nanyi mtayafanya." Wewe amini Hilo kwa moyo wako wote.

232 Yule mtu anayesimama kule nyuma ana shida kwenye nyonga yake. Wewe amini Hilo kwa moyo wako wote. Huwezi kuingia katika mstari wa maombi, bali unaweza kurudi na kuketi chini, itaondoka. Na si kansa. Rudi ukaketi chini, yote imekwisha. Sijapata kumwona mtu huyo maishani mwangu. Kama hatufahamiani, ndugu, inua mkono wako. Kama hatufahamiani. . .Kuna shida gani, yeye ameponywa! Yesu Kristo amekuponya.

Huku madhabahuni, mnaamini?

233 Na wewe je? Hatufahamiani, sikujui mimi. Mungu anakujua. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini Ujumbe huu ninaohubiri? Vipi kama ningalikwambia ugonjwa wako wa mgongo utakuacha? Unaliamini kwa moyo wako wote? Vema, Bw. Burkhart, wewe rudi Ohio, umeponywa. Yesu Kristo anakuponya.

234 Huko hapa kwa ajili yako, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Ni mwanamke. Naye ametoka Ohio, pia, hiyo ni kweli, jina ni Alice McVan. Hiyo ni kweli. Alifanyiwa upasuaji. Hiyo ni kweli. Ugonjwa wa tumbo na shida ya akina mama na

wasiwasi. Hiyo ni kweli? Amini tu naye ataponywa. Endelea na uamini kwa moyo wako wote. Amini kwa moyo wako wote, atapokea.

235 U hali gani? Sikujui mimi, hatufahamiani. Hiyo ni kweli? Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini ya kwamba tumepata ushindi katika Kristo? Kama unaamini, na wasiwasi wako na shida zako na mambo uliyo nayo, basi, Bibi Allen, unaweza kurudi nyumbani kwako na ukaponywe.

236 Ninaamini ya kwamba hatufahamiani, sivyo? Sijapata kukuona hapo kabla. Hii ndiyo mara ya kwanza tumekutana, hatufahamiani. Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaamini hivyo? Unaugua ugonjwa wa figo. Hiyo ni kweli, sivyo? Hutoki hapa, umetoka Kusini. Unawaombea watoto wako wasiookolewa. Huyo ni mume wako nyuma yako. Ana mtu fulani moyoni mwake asubuhi ya leo, rafiki anayemwombea. Aisee, ninamwona mtu fulani, wewe ni—wewe ni rafiki ya mama na baba yangu. Mtu anayekuja hapa jina lake L. C. ama S. T., ama kitu kama hicho, S. T. ama kitu fulani, huyo—huyo ni mwanao. [Ndugu Neville anasema, "J. T."—Mh.] J. T. . . Haya basi, S. T. La, si J. T., najua. Ni mtu mdogo, mwenye nywele nyeusi, nilimwona amesimama papa hapa mbele mahali alipo sasa. Rudi nyumbani, umepata ombi lako. Rudi nyumbani.

237 Je! mtu huyo yupo hapa asubuhi ya leo, mtu aliyetoka huko Georgia? Naam. T. S. Naam. Sijapata kuwaona baba na mama yako maishani mwangu, nawe unajua hiyo ni kweli, bali nilikuona hapa juu, papa hapa mbele yao wakati uo huo. Nilijua ni wewe. Umepata haja yako, usitilie shaka.

238 Nyote mnaamini, kwa moyo wenu wote? Sasa, ni wangapi? Kila mmoja wenu ninyi nyote yumo katika Kristo. Mnasema, "Hiyo ni Injili?" Hivyo ndivyo Yesu Kristo alivyofanya hasa. Hivyo ndivyo mitume walivyofanya hasa. Hivyo ndivyo Ireneo na hao wengine walivyofanya. Hivyo kabisa.

Unaliamini Hilo? Basi inamisha kichwa chako.

239 Njoo hapa, mzee. Kuna watu wengi mno wa kupitia kwenye mstari huo wote namna hiyo. Tumewachukua wawili ama watatu hapo ndani. Shuka uje moja kwa moja hapa. Huyu Ndugu yangu Neville ni mtu wa Mungu. Ninaamini.

240 Tutapitia kwenye mstari huu hapa na kuwaombea watu hawa, kuwawekea mikono. Nyote mnaamini watapata afya, kila mmoja wenu? Kila mtu hapa ndani ataamini Hilo? Basi inamisha kichwa chako sasa, tuko katika Kanisa lililoshinda.

241 Bwana Yesu, ninamjua ndugu huyu, hiyo ndiyo sababu sikumwambia kitu kulihusu. Ninajua anachohitaji. Ninaomba ya kwamba utamponya, Bwana, na kumpa haja yake. Katika Jina la Yesu Kristo.

242 Baba wa Mbinguni, huku mikono imewekwa juu ya maskini ndugu huyu, asubuhi ya leo, tunauombea ukombozi wake katika Jina la Yesu. Amina.

243 Loo, unaninii . . .

Baba wa Mbinguni, mpe Dada yetu Dauch hapa, dada mpendwa, ambaye amekuwa ni rafiki halisi kwetu hapa, kwa familia yangu na wapendwa wetu. Tunaamini ya kwamba yeye na mume wake ni watoto Wako. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utamjalia haja yake asubuhi ya leo. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

244 Mungu, katika Jina la Yesu, mbariki Dada yetu Bruce. Tunajua, Bwana, ya kwamba yeye ni mtumishi Wako. Tunaomba ya kwamba utamtimizia haja ya—yake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

245 Ee Baba wa Mbinguni, tukitambua ya kwamba—ya kwamba Wewe pekee unaweza kumponya Dada Blankco, tunaomba ya kwamba utambariki na kumtimizia ombi hili, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

246 Baba wa Mbinguni, juu ya dada yetu tunaiweka mikono yetu katika Jina la Yesu Kristo, kuombea ukombozi wake kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

247 "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," nasi tunaiweka mikono yetu juu ya dada huyu ambaye atapona. Katika Jina la Yesu, lijalie, Bwana. Wakati mwili huu wenye wasiwasi, unaotetemeka, ukisimama hapa, Bwana, chini ya nguvu za Roho Mtakatifu, na umechoka, bali Wewe ni Mungu. Mponye msichana huyu, ninaomba, katika Jina la Yesu Kristo.

248 Mwenyezi Mungu, mpe ndugu yetu haja yake. Tujalie, Baba. Tunamwekea mikono yetu na kumlaani adui, hao ambao wangeitia sumu nafsi yake, ama kutia do—doa jeusi mbele yake. Jalia ainuke kwa ushindi juu ya huo asubuhi ya leo, Bwana, na kutambua mahali pake katika Kristo Yesu. Na kwa hiyo atapata kile alichoomba, katika Jina la Yesu.

249 Baba yetu wa Mbinguni, huku mikono imewekwa juu ya ndugu huyu, katika Jina la Yesu Kristo, jalia haja yake. Amina.

250 Maskini msichana huyu kipenzi, Baba, katika Jina la Yesu jalia Bwana amrehemu, kwa ajili ya Utukufu wa Mungu tunaombea ukombozi wake.

251 Mungu, tunajua kilio cha moyoni cha mama huyu na kilio cha binti yake. Mungu, mjalie imani asubuhi ya leo, na halafu uitumie sasa hivi, tukijua ya kwamba ana mamlaka juu yake. Nalo litatendeka, katika Jina la Yesu Kristo.

252 Mungu, mponye mvulana huyu mdogo, tunaomba katika Jina la Yesu Kristo.

253 Mungu, Baba yetu, tunaweka mikono juu ya dada yetu na kuomba asubuhi ya leo umtimizie haja yake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

254 Baba yetu wa Mbinguni, wakati msichana huyu anapokuja kuchukua mahali pake kwa ajili ya uponyaji, tunaweka mikono juu yake na kuombea uponyaji wake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

255 Juu ya mtoto huyu mdogo anayependeza tunaiweka mikono yetu, katika Jina la Yesu Kristo, tunaombea uponyaji.

256 Kwa Jina la Yesu Kristo, huku mikono ikiwa juu ya dada yetu, naomba umponye sasa.

257 Baba yetu, uliye Mbinguni, Jina Lako litukuzwe, juu ya ndugu huyu tunaiweka mikono yetu. Katika Jina la Yesu Kristo, jalia aliamini. Amina.

258 Baba wa Mbinguni, juu ya ndugu yetu shujaa hapa, mtumishi Wako, mtu wa Mungu, tunaweka mikono juu yake kwamba haja yake itimizwe. Katika Jina la Yesu Kristo na achukue mahali pake sasa. Sasa, huyu hapa mwana wa Mungu, katika utukufu wa wakati, Ee Bwana.

259 Baba wa Mbinguni, juu ya maskini dada yetu ambaye ametoka katika giza kuu apate kutembea katika Nuru, jalia, Bwana, kwamba maskini nafsi yake shujaa itainuliwa asubuhi ya leo, mpaka kwenye mazingira ya Mbinguni. Na umtimizie haja ya—yake, katika Jina la Yesu. Amina.

260 Baba wa Mbinguni, juu ya ndugu yetu hapa tumeweka mikono katika Jina la Bwana Yesu, tukiomba ajaliwe haja hii. Katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Amina.

261 Baba yetu wa Mbinguni, tunaweka mikono juu ya mtoto mchanga wa Dada yetu, na kuomba ya kwamba ajaliwe haja yake, Baba, tunapoiweka mikono yetu juu yake katika Jina la Yesu Kristo.

262 Baba yetu wa Mbinguni, tunaiweka mikono juu ya dada yetu, katika Jina la Yesu Kristo. Jalia haja yake itimizwe, katika Jina la Yesu. Amina.

263 Baba yetu wa Mbinguni, wakati dada yetu akipitia kwenye mstari huu na kuacha . . . tunaweka mikono yetu juu yake, jalia Kristo wa Mungu aje karibu sasa na kuulaani ugonjwa huu na ampe afya. Amina.

264 Baba wa Mbinguni, juu ya ndugu yetu, tunaweka mikono juu yake na kuomba kwamba katika Jina la Yesu Kristo, kwamba utamponya katika Jina la Yesu. Amina.

265 Baba wa Mbinguni, juu ya msichana huyu tunaiweka mikono yetu, na kumwomba Bwana wetu wa thamani. Katika Jina la Yesu Kristo, tunaombea uponyaji wake. Amina.

266 Bwana wetu wa thamani, tunaweka mikono juu ya ndugu yetu, katika Jina la Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, ambaye Kwake sisi ni zaidi ya washindi. Nasi tunaomba ya kwamba utamjalia ndugu yetu haja yake, katika Jina la Yesu. Amina.

267 Baba yetu, juu ya ndugu ya mjakazi wetu, maskini askari huyu wa Msalaba, ninaomba, Mungu, ya kwamba Roho Wako aje juu yake na kumjalia haja yake. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

268 Baba yetu wa Mbinguni, juu ya askari huyu shujaa wa Msalaba, yeye amelitetea Neno Lako katika—katika nyakati za ukosoaji na kadhalika, na bado analitetea Neno, akaondoka akiwa ni zaidi ya mshindi katika Kristo Yesu. Mjalie haja yake, Baba. Ninaomba maombi yangu na kumpa kutoka kwenye baraka Zako, Bwana, kwamba utamponya na kumtimizia haja yake. Katika Jina la Yesu. Amina.

269 Baba wa Mbinguni, mtoto huyu mchanga hawezi kuishi nje ya Mungu, bali Mungu anaweza kumponya. Ninaweka mikono juu yake na kumlaani adui, katika Jina la Yesu Kristo. Mbariki mtoto huyu, na umjalie kufanikiwa katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

270 Baba wa Mbinguni, kwa dada yetu, ambaye tunaweka mikono juu yake katika Jina la Yesu Kristo, maskani iliyoshinda ya Mungu iliyofanyika mwili na kukaa miongoni mwetu. Jalia kupitia Jina Lake, Jina la haki la yule Mwana wa Mungu, Yesu Kristo, mpe dada yetu haja yake. Amina.

271 Dada yetu Kidd, ubarikiwe moyo wako. Baba yetu wa Mbinguni, wakati nikimshika mzee huyu na mwanamke mikononi mwetu hapa, ambaye ameihubiri Injili nilipokuwa mvulana mdogo tu, siku chache zilizopita alilala akifa kwa kansa; nikikimbia kumfikia, nazo nguvu za Mungu zikashuka juu ya mtu mwenye umri wa miaka themanini na kumponya, hata madaktari walinyamaza kimiujiza, wasingeweza kufahamu hilo. Ninaomba ya kwamba utamjalia haja yake asubuhi ya leo. Maskini mke wake aliyebarikiwa, Bwana, ambaye amefua kwenye ubao apate kumtuma mumewe hudumani akahubiri Injili hii ina—inayotokwa na Damu ya Yesu Kristo. Tujalie, Bwana.

272 Mbariki mwana wao, Junior, Bwana. Tunaomba ya kwamba utamponya na kumweka akiwa na nguvu, Bwana. Yeye ndiye msaidizi wao anayewabeba kutoka mahali hadi mahali, kuweka leso. Ingawa ni wazee sana wasingeweza kuingia hudumani tena, bali wao huenda kutoka hospitalini hata manyumbani, wakiweka leso juu ya wagonjwa. Mungu, Wewe utaheshimu hilo, ninajua utaliheshimu. Wabariki na uwape nguvu kwa ajili ya siku zingine nyingi, Baba. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

273 Ubarikiwe. Itatendeka, Ndugu Kidd, itatendeka. [Ndugu na Dada Kidd wanazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Mungu asifiwe. Amina. Naam, yule tuliyemwombea kwa simu.

274 Mwanamume na mwanamke wenye umri wa miaka themanini, na zaidi, hawawezi kwenda kwenye huduma na kusimama mimbarani, wazee sana wakati huu kuhubiri namna hiyo, bali hata hivyo wataagizia huku na kupata vifurushi vya leso za maombi na kuwapelekea wagonjwa na wanaoteseka, wanazipeleka hospitalini na kila kitu namna hiyo. Kuziweka juu ya ninii. . .Hawawezi tena kutoka na kuisaidia huduma kwa njia hiyo, bali wanaendelea vizuri wawezavyo. Linapaswa kutufanya sisi vijana tujionee aibu. Hiyo ni kweli, kutenda jambo kwa ajili ya Kristo.

275 Kumbukeni, mzee huyu hapa, Ndugu Kidd, alikuwa akiihubiri Injili kabla sijazaliwa. Hiyo ni kweli, huko nje akiwaombea wagonjwa, askari hodari. Na hapa, mzee, je! una umri gani, Ndugu Kidd? Umri wa miaka themanini na moja, na angali akiufuatilia Ufalme wa Mungu! Ni mzee sana hata hawezi kusimama mimbarani na kuushikilia ujumbe namna hiyo, bali ataenda hospitalini, kando ya vitanda, ambapo ana mvulana ambaye humpeleka kila mahali kwa gari. Nao hawawezi kutembea, kwa hiyo wanambeba tu kwa gari na kuwapeleka mahali fulani, na hao wawili, mtu na mke wakongwe, wanaingia mle na kuwawekea leso.

276 Walikuwa na mpendwa mahututi hivi majuzi, msichana, ambaye ndiyo kwanza waniambie habari zake. Tukawaombea, mjukuu, wakaenda kumwekea. . .Mtoto huyo ameamka sasa. Mungu asifiwe!

277 Ndugu Kidd, waliniita hapa hivi majuzi, karibu miaka miwili iliyopita, nadhani, imekuwa, kwamba alikuwa na kansa kwenye tezi kibofu, kwenye umri wa kama miaka sabini na minane, ama themanini, karibu miaka themanini, akiwa na kansa kwenye tezi kibofu. Daktari aliiweka kando tu, hakuna kitu kingaliweza kufanywa. Tukafanya hima, mimi na Billy tukashika zamu kuendesha gari, kufika mahali pale alipokuwa. Ndipo Roho Mtakatifu akatwambia twende asubuhi hiyo. Kwa kawaida hatufanyi hivyo tusipoongozwa kulifanya. Ndipo Roho Mtakatifu akasema, "Nendeni," nasi tukaondoka kuelekea kule na kumwekea mzee huyo mikono, kumwombea. Nao madaktari hawawezi kuona dalili yake popote. Utukufu kwa Mungu! Loo! Mbona? Mahali petu ni katika Kristo Yesu, alipaa juu ya magonjwa yote na nguvu zote za adui.

278 Loo, hivi hamna furaha kwa ajili Yake?

> Wapo watu karibu kila mahali,
> Ambao mioyo yao inawaka moto
> Kwa Moto huu ulioshuka kwenye Pentekoste,

Uliowasafisha na kuwafanya safi;
Loo, unawaka sasa moyoni mwangu,
Loo, utukufu kwa Jina Lake!
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Ingawa huenda watu hawa wasielimike wakawa,
Wala kujivunia sifa za ulimwengu,
Wote wamepokea Pentekoste yao,
Wakabatizwa katika Jina la Yesu;
Nao wanatangaza sasa, mbali na kwa mapana pia,
Nguvu Zake zingali ni zile zile,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

279 Ni wangapi walio mmoja wao? Inueni mikono yenu sasa:

. . . wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Loo, mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Sasa njoo, ndugu yangu, itafute baraka hii
Itakayousafisha moyo wako kutoka dhambini,
Itakayofanya kengele za shangwe zianze kulia
Na itaendelea kuiwasha moto nafsi yako;
Loo, inawaka sasa moyoni mwangu,
Utukufu kwa Jina Lake,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao; Haleluya!
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Walikuwa wamekusanyika kwenye chumba cha juu,
Wote wakiomba katika Jina Lake,

Walibatizwa kwa Roho Mtakatifu,
Ndipo nguvu za utumishi zikaja;
Sasa yale aliyowafanyia siku hiyo
Atakufanyia yayo hayo,
Na nina furaha sana kwamba ninanaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao; Haleluya!
Mmoja wao, mmoja wao,
Loo, nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

280 Sasa wakati tukiuvumisha, hebu na tupeane tu mikono sisi kwa sisi. Tuseme:

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao; Haleluya!
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

281 Nawe je? Semeni, "Amina!" [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.]

Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

282 Naweza kurudia aya hii tena?

Ingawa huenda watu hawa wasielimike wakawa. (Hawana D.D., ma-Ph.D. zozote kubwa mno, mnaona, hawana kitu chochote kikubwa mno, mnaona.)

Huenda watu hawa wasijifunze wakawa,
Wala kujivunia sifa za ulimwengu, (dhehebu fulani kuu)
Wote wamepokea Pentekoste yao,
Kila mmoja wao amebatizwa katika Jina la Yesu;
Nao wanatangaza sasa, mbali na kwa mapana pia,
Nguvu Zake zingali ni zile zile,
Nina furaha sana kwamba ninaweza kusema mimi ni mmoja wao.

Mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao;
Mimi ni mmoja wao, mmoja wao,
Nina furaha sana kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao.

Loo, nisingeacha mahali hapa pa thamani kwa ajili ya mamilioni yote ya dhahabu ya dunia hii,
Ingawa mjaribu ameninii...mara nyingi amejaribu kunishawishi,
Bali mimi ni salama katika banda la Mungu, nina furaha katika upendo Wake na neema,
Nami ninaishi katika maeneo ya Haleluya!

283 Loo, jamani! Nina furaha sana kwa ajili ya hilo. Sivyo nanyi? Hivi hamna furaha kuwa mmoja wao? Mmoja wao tu, mmoja wa hao watu wanyenyekevu ambaye ndio kwanza ajifanye tupu kabisa, akashuka chini (sio mbele ya sanamu fulani), mbele za Mungu aliye hai, (sio mbele ya dhehebu na kuweka jina lako kwenye kitabu), mbele ya Mungu aliye hai, (sio kukariri kanuni fulani za imani), bali kuliacha Neno lifanyike mwili ndani yako. Unaona, jambo ndilo hilo. Na kujinyenyekeza, na halafu kupitia hapo akakuinua juu, (sio upate kuwa mkaidi, mwenye kujivuna, kusema "Mimi ni *hiki*, *kile* ama *kinginecho*"), bali katika unyenyekevu, utamu, na "je! alipataje kumwokoa mnyonge kama mimi, na alipataje kufanya hivyo?" Hivyo ndivyo Mkristo halisi anavyojisikia. Hamwamini hilo? Loo, Yeye ni halisi sana!

Halisi, halisi, Yeye ni halisi sana kwangu!
Loo, halisi, halisi, Yeye ni halisi sana kwangu!
Ingawa watu wengine wanamtilia shaka, siwezi kuishi bila Yeye,
Hiyo ndiyo sababu ninampenda, Naye ni halisi sana kwangu!

Halisi, Yeye ni halisi sana kwangu! (Uimbeni!)
Halisi, halisi, Yeye ni halisi sana kwangu!
Ingawa watu wengine wanamtilia shaka, bali mimi siwezi kuishi bila Yeye,
Hiyo ndiyo sababu ninampenda, Naye ni halisi sana kwangu!

284 Loo, loo, ninafurahia hilo sana! Naam, bwana. Loo, nina furaha sana kwa ajili ya njia hii kuu ya Injili ya kale, kuishi katika njia hii tukufu ya Injili ya kale.

285 Sasa, enyi marafiki, mpaka tutakapokutana kwenye Kiti cha Enzi cha Kristo tena, mnapoomba, nikumbukeni. Na Mungu ambariki kila mmoja wenu. Siwezi kusema samahani niliwaweka hapa.

286 Sasa, kwenu ninyi mlio na leso zilizowekwa hapa, niliziwekea tu mikono wakati tukiwaombea wagonjwa, kama mliniona nikifanya hivyo mara Roho aliposhuka. Sikuingia katika maono mengi mno, kwa kuwa mimi ni dhaifu, nimechoka, mwajua, nimekuwa hapa yapata saa mbili ama tatu sasa, nikihubiri, nami nilianza tu kupata wachache mstarini kusudi mpate kuona ya kwamba Mungu ni Mungu. Mnaona? Yasiyowezekana, kile kitendawili, kwamba mambo yasiyotafutika . . . Ibilisi . . .

287 Sasa, kumbukeni, kila mmoja wenu ana nguvu katika Kristo. Huna nguvu, una *mamlaka*, mamlaka yako. Umeinuliwa tu, juu sana; sio ukajiinue juu, bali Kristo amekuinua juu. Kadiri Kristo anavyokuinua, ndivyo unavyotaka kushuka chini zaidi, unaona, utajisikia mnyenyekevu sana. Kwa hiyo angewezaje kumwokoa mnyonge kama mimi, alifanyaje hilo kamwe? Lakini alilifanya, na kwa hiyo ninashukuru kwa ajili yake. Amina! Vema sana!

> Tukiliinamia Jina la Yesu,
> Tukisujudia miguuni Pake,
> Tutamvika taji Mbinguni kama Mfalme wa Wafalme,
> Hapo safari yetu itakapokamilika.
>
> Jina la thamani (Jina la thamani!), Ee ni tamu jinsi gani!
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
> Jina la thamani (Loo, Jina la thamani! Yeye si ni wa ajabu?)
> Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

288 Sasa, sikilizeni, msisahau jambo hili. Ninyi imbeni pambio, hebu niimbe kifungu chake. Mnaona? Sijui kama ninaweza kukumbuka kifungu chake ninachotaka kuimba, ndilo jambo la pili.

> Tukiliinamia Jina la Yesu,
> Tukisujudia miguuni Pake,
> Tutamvika taji kama Mfalme na Wafalme wa Mbinguni,
> Hapo safari yetu itakapokamilika. (Mnaona?)
>
> Peleka Jina la Yesu,
> Kama ngao ya kila mtego;
> Majaribu yakikuzunguka,
> Taja tu Jina hilo katika maombi.

Hivyo tu. Inua mkono huo na usikilize breki zikilia! Unaona? Unaona?

> Taja Jina hilo katika maombi.

Jina la thamani, Ee ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani (Loo, Jina la thamani!), Ee ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

289 Hebu tuseme hivyo tena, sisi sote pamoja. Unasema nini? Hebu tukichukue kifungu hicho tena, kuhusu, "Peleka Jina la Yesu, kama ngao ya kila mtego." Hebu tuuimbe sasa huku macho yetu yamefumbwa.

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao ya kila mtego;

Sasa sikilizeni. Unafanya nini?

Majaribu yakikuzunguka,

Inakupasa kufanya nini?

Taja Jina hilo katika maombi.

Jina la thamani (Jina la thamani!), Ee ni tamu jinsi gani!
Tumaini la duniani na . . .

[Ndugu Neville anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] (Sifanyi hivyo. La, kidogo ni—nimepwelewa na sauti, nimepwelewa kidogo na sauti, kwa hiyo sitasema . . .?. . . Unataka kuwaacha wafumukane . . .?. . . La, ni vema, endelea tu moja kwa moja, hilo ni sawa.)

Tumaini la duniani na . . .

Ndugu Neville, mchungaji wenu, sasa.

*Ukristo Dhidi Ya Uabudu Sanamu* SWA61-1217
(Christianity Versus Idolatry)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulihubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 17 Desemba, 1961, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila jitihada imefanywa kuuhamisha ujumbe huu wa sauti kutoka kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2018 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org